**ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI**
**SPIKA – MHE. PANDU AMEIR KIFICHO**

| | |
|---|---|
| 1.Mhe. Kamal Basha Pandu | Naibu Spika/Jimbo la Rahaleo. |
| 2.Mhe. Ali Mzee Ali | Mwenyekiti wa Baraza/Uteuzi wa Rais. |
| 3. Thuwaibah Edington Kissasi | Mwenyekiti wa Baraza/Nafasi za Wanawake. |
| 4.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha | MBM/Waziri Kiongozi/ Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Jimbo la Mwanakwerekwe. |
| 5.Mhe. Ali Juma Shamuhuna | MBM/Naibu Waziri Kiongozi/Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo/ Jimbo la Donge. |
| 6.Mhe. Abubakar Khamis Bakary | Kiongozi wa Upinzani/"Waziri Kivuli"–Afisi ya Waziri Kiongozi/Jimbo la Mgogoni. |
| 7.Mhe. Haji Omar Kheri | Mnadhimu wa Upande wa Serikali/Jimbo la Tumbatu. |
| 8.Mhe. Haji Faki Shaali | "Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Katiba na Utawala Bora/Mnadhimu wa Upande wa Upinzani/Jimbo la Mkanyageni. |
| 9.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini | MBM/Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi/ Jimbo la Dimani. |
| 19.Mhe. Ramadhan Abdulla Shaaban | MBM/Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora/Uteuzi wa Rais. |

| | |
|---|---|
| 11.Mhe. Suleiman Othman Nyanga | MBM/Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi Vya S.M.Z./Jimbo la Jang'ombe. |
| 12.Mhe. Hamza Hassan Juma | MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/ Jimbo la Kwamtipura. |
| 13. Mhe. Machano Othman Said | Waziri wa Nchi, (AR) Mawasiliano na Uchukuzi./Jimbo la Chumbuni. |
| 14. Mhe. Br.Gen. Adam C. Mwakanjuki | MBM/Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Uteuzi wa Rais. |
| 15.Mhe. Samia Suluhu Hassan | MBM/Waziri wa Utalii/Biashara na Uwekezaji/Nafasi za Wanawake. |
| 16.Mhe. Burhan Saadat Haji | MBM/Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/ Jimbo la Kikwajuni. |
| 17.Mhe. Asha Abdalla Juma | MBM/Waziri wa Kazi Maendeleo ya Vijana,Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais. |
| 18.Mhe. Haroun Ali Suleiman | MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Makunduchi. |
| 19.Mhe. Sultan Moh'd Mugheiry | MBM/Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/ Uteuzi wa Rais. |
| 20.Mhe. Mansoor Yussuf Himid | MBM/Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Kiembesamaki. |
| 21.Mhe. Zainab Omar Moh'd | MBM/Waziri wa Nchi (AR) Kazi Maalum/ Nafasi za Wanawake. |
| 22.Mhe. Idi Pandu Hassan | Mwanasheria Mkuu wa Serikali. |

| | |
|---|---|
| 23. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo | Naibu Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo/Jimbo la Mpendae. |
| 24. Mhe. Mzee Ali Ussi | Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chaani. |
| 25. Mhe. Khatib Suleiman Bakari | Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Bububu. |
| 26.Mhe. Khamis Jabir Makame | Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mtoni. |
| 27.Mhe. Shawana Bukheti Hassan | Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Dole. |
| 28.Mhe. Tafana Kassim Mzee | Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Uzini. |
| 29.Mhe. Zahra Ali Hamad | "Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/Nafasi za Wanawake. |
| 30.Mhe. Zakiya Omar Juma | "Waziri Kivuli"-Wizara ya Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Nafasi za Wanawake. |
| 31.Mhe. Said Ali Mbarouk | "Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) na MBLM Fedha na Uchumi/Jimbo la Gando. |
| 32.Mhe. Abdulla Juma Abdulla | "Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Tawala za Mikoa na Vikosi Vya SMZ/Jimbo la Chonga. |
| 33.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak | "Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) Kazi Maalum/Nafasi za Wanawake. |

| | |
|---|---|
| 34.Mhe. Hamad Masoud Hamad | “Waziri Kivuli”–Wizara ya Maji,Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Ole. |
| 35.Mhe. Omar Ali Shehe | “Waziri Kivuli”–Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chake-Chake. |
| 36.Mhe. Rashid Seif Suleiman | “Waziri Kivuli”–Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Ziwani. |
| 37.Mhe. Mohamed Ali Salim | “Waziri Kivuli”–Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mkoani. |
| 38.Mhe. Asaa Othman Hamad | “Waziri Kivuli”–Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Wete. |
| 39.Mhe. Aziza Nabahan Suleiman | “Waziri Kivuli”–Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Nafasi za Wanawake. |
| 40.Mhe. Najma Khalfan Juma | “Waziri Kivuli”–Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo/Nafasi za Wanawake. |
| 41.Mhe. Muhyddin Moh’d Muhyddin | “Waziri Kivuli”–Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji/Jimbo la Mtambile. |
| 42.Mhe. Abdulla Mwinyi Khamis | Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja. |
| 43. Mhe. Abass Juma Muhunzi | Jimbo la Chambani. |
| 44.Mhe. Ali Abdalla Ali | Jimbo la Mfenesini. |
| 45.Mhe. Ali Denge Makame | Jimbo la Amani. |
| 46.Mhe. Ali Haji Ali | Jimbo la Mkwajuni. |

| | |
|---|---|
| 47.Mhe. Ali Moh'd Bakari | Jimbo la Tumbe. |
| 48.Mhe. Ali Suleiman Ali | Jimbo la Kwahani. |
| 49.Mhe. Ame Mati Wadi | Jimbo la Matemwe. |
| 50.Mhe. Ame Ussi Juma | Jimbo la Nungwi. |
| 51.Mhe. Amina Iddi Mabrouk | Nafasi za Wanawake. |
| 52.Mhe. Anaclet Thobias Makungila | Jimbo la Fuoni. |
| 53. Mhe. Asha Moh'd Hilal | Jimbo la Magogoni. |
| 54.Mhe. Ashura Abeid Faraji | Nafasi za Wanawake. |
| 55.Mhe. Bihindi Hamad Khamis | Nafasi za Wanawake. |
| 56.Mhe. Dadi Faki Dadi | Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Pemba. |
| 57.Mhe. Fatma Abdalla Tamim | Nafasi za Wanawake. |
| 58.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji | Jimbo la Mji Mkongwe. |
| 59.Mhe. Haji Mkema Haji | Jimbo la Koani. |
| 60.Mhe. Hasnuu Moh'd Haji | Uteuzi wa Rais. |
| 61.Mhe. Hija Hassan Hija | Jimbo la Kiwani. |
| 62.Mhe. Major Juma Kassim Tindwa | Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Pemba. |
| 63. Mhe. Juma Duni Haji | Uteuzi wa Rais |
| 64.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk | Jimbo la Kitope. |
| 65.Mhe. Mkongwe Nassor Juma | Nafasi za Wanawake. |
| 66.Mhe. Moh'd Kombo Mkanga | Jimbo la Chwaka. |

| | |
|---|---|
| 67.Mhe. Mustafa Moh'd Ibrahim | Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Unguja. |
| 68.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi | Nafasi za Wanawake. |
| 69. Mhe. Nassor Ahmed Mazrui | Uteuzi wa Rais |
| 70.Mhe. Omar Ali Jadi | Jimbo la Kojani. |
| 71.Mhe. Pembe Juma Khamis | Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Unguja. |
| 72.Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu | Jimbo la Muyuni. |
| 73.Mhe. Raya Suleiman Hamad | Nafasi za Wanawake. |
| 74.Mhe. Said Khelef Ali | Jimbo la Bumbwini. |
| 75.Mhe. Salim Abdulla Hamad | Jimbo la Mtambwe. |
| 76.Mhe. Salmin Awadh Salmin | Jimbo la Magomeni. |
| 77.Mhe. Subeit Khamis Faki | Jimbo la Micheweni. |
| 78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis | Jimbo la Konde. |

| | |
|---|---|
| **Ndg. Ibrahim Mzee Ibrahim** | **Katibu wa Baraza la Wawakilishi.** |

**Kikao cha Kumi na Moja – Tarehe 24 Juni, 2010**

*(Mkutano ulianza saa 3:00 asubuhi)*

**DUA**

*Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua*

**MASWALI NA MAJIBU**

**Nam. 64**

**Skuli ya Mafunzo ya Uuguzi Pemba**

**Mhe. Hija Hassan Hija –** Aliuliza:-

Hivi karibuni *Zanzibar Commercial Institute* imeanzisha Skuli ya Kufunza Wauguzi (*School of Nursing*), kisiwani Pemba. Skuli hiyo tayari imesajili wanafunzi wapatao 152. Miongoni mwao wanafunzi 100 ni wa cheti na 52 ni diploma.

(a) Je, skuli hiyo inatambuliwa rasmi na serikali pamoja na vyombo vinavyosimamia taasisi (*regulatory authorities*) za elimu nchini Tanzania?

(b) Je, kwa sasa Zanzibar ina upungufu wa wauguzi wangapi na kama upungufu upo pale watakapomaliza wale wanaotoka *Zanzibar Commercial Institute* wataajiriwa lini ili kuziba pengo hilo?

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii –** Alijibu:-

Mhe. Spika kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Namba 64 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii inayo taarifa ya kuanzishwa Skuli ya Wauguzi huko Pemba.

Katika kutaka kuitambua skuli hiyo, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii iliutaka Uongozi wa Skuli hiyo kufanya mambo kadhaa yakiwemo:-

(i) Kuwasilisha wizarani taarifa za walimu, vifaa na jengo litalotumika;

(ii) Kutoanzisha masomo mpaka skuli ikaguliwe na kuidhinishwa;

(iii) Mtaalamu wa mafunzo yatakayosomeshwa; na

(iv) Sifa za wanafunzi na vyeti vitakachotolewa.

Mhe. Spika, hivi karibuni maofisa watatu wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii walitembelea skuli hiyo na kukuta masomo yameshaanza kukiwa na wanafunzi 94 wa masomo ya uuguzi , Ukunga wa Afya ya Jamii (*PHNB*) na 77 wa uuguzi. Chuo hicho kimekutikana hakina walimu wa kudumu, pia hakikuwa na sifa za kusomesha, darasa halina meza, viti na halina sifa za kusomeshea.

Walimu wamiliki wa skuli hiyo walianzisha masomo kabla ya kukaguliwa. Kwa upande wa hapa Unguja mpaka leo hajawa tayari kukaguliwa kwa masomo anayosomesha. Kwa hivyo, mmiliki ameshaandikiwa barua kusitisha masomo hayo mara moja. Wizara hakikitambui chuo hicho na wala wahitimu wa chuo hicho hawatabuliwi.

Mhe. Spika, tunapenda watu binafsi waanzishe skuli kama hizo, lakini ziwe na sifa na zifuate kanuni na taratibu zilizowekwa na serikali.

b) Mhe. Spika, kwa sasa Zanzibar inao upungufu wa fani ya Wauguzi 650, ambapo wanafunzi wanaomaliza fani ya Uuguzi kutoka vyuo mbali mbali vinavyotambulika hapa Tanzania na kuthibitishwa na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, wanaweza kuajiriwa ili kuziba pengo hilo.

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Spika, baada ya majibu ya Mhe. Naibu Waziri nataka nimuulize swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b). Amekiri kwamba chuo hicho kipo Pemba na kinaendelea masomo yake.

(a) Kwa hivyo, nataka kujua ni chombo gani Zanzibar au Tanzania chenye mamlaka ya kutoa leseni ya chuo kama hicho.

(b) Zipo taarifa kwamba sababu kubwa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, wamekataa kukitambua chuo hicho kwamba kuna mgongano baina ya chuo hicho na Chuo cha Afya Mbweni. Je, hiyo ni kweli?

(c) Kwa nini chuo hicho hakitambuliki na serikali, lakini baadhi ya walimu wa Chuo cha Afya Mbweni inasemekana ndio wanaosomesha chuo hicho Pemba.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii:** Mhe. Spika, chombo chenye mamlaka ya kutoa leseni kwa hapa Zanzibar ni Bodi au Baraza la Wauguzi, ndilo linalotoa mamlaka kwa ajili ya mafunzo ya hapa Zanzibar.

Kuhusu mgongano wa Chuo cha Afya Mbweni na hiki kilichoanzishwa, Mhe. Spika sisi hatuna taarifa hii na wala hakuna mgongano. Nadhani kinachoonekana mhusika yeye alikwenda kwenye Baraza la Wauguzi na kutaka kuanzisha chuo na alipewa maelekezo. Lakini hakuyafuata na badala yake alikurupuka kuanzisha chuo bila ya kufuata utaratibu, ndio maana maafisa wakamua kwenda kumkagua baada ya kupata hizi taarifa. Kwa hivyo, mgongano wa Chuo cha Afya Mbweni na hiki kilichoanzishwa haupo na wala hakuna taarifa hiyo.

Mhe. Spika, kuhusu baadhi ya walimu wa Chuo cha Afya Mbweni ndio wanaokwenda kusomesha huko. Kwa kweli taarifa hiyo nataka kukiri Mhe. Spika kuwa tumeipata kwa kuwa kuna walimu ambao wamechukua likizo bila ya malipo ndio wapo huko. Lakini hawakidhi na wala hawatoshelezi, kwa sababu wao wapo kama ni *part time* tu. Kwa hivyo, huo si utaratibu wa kuanzisha chuo mtu hatakiwi kufanyakazi kwa *part time*, isipokuwa anatakiwa awepo pale *full time*. Kwa maana hiyo, bado tunasema chuo hakina sifa. Kwa utaratibu uliopo ni kusimamisha mafunzo.

**Mhe. Ame Mati Wadi:** Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa chuo hicho kitakapokuwa kinaendelea ni mkombozi, kwa sababu tukitaka tusitake wauguzi hawatoshi Zanzibar. Kwa kuwa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, imetoa ruhusa kwamba mfanyakazi atakapomaliza muda wake wa kazi anayo haki ya kutafuta maeneo mengine ya kuongeza kipato.

Hivi naomba nimuulize Mhe. Waziri ambaye ndiye mwenye kutoa muongozo. Mambo gani ambayo yamekwamwisha sifa ya kutokufaa kuendelea na kutoa mafunzo, majengo, taaluma au wanafunzi ambao wanashiriki hapo hawana sifa kamili za kufundishwa?

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii:** Mhe. Spika, kwenye jibu mama nimejibu kwamba kuna mambo ambayo mmiliki alitakiwa mmiliki wa chuo hiki ayakamilishe ndio chuo kiweze kufunguliwa.

(a) Kuwasilishe wizarani taarifa za walimu, vifaa na jengo litakalitumika;

(b) Kutokuanzisha masomo mpaka skuli ikaguliwe;

(c) Mitaala ya mafunzo nayo yaweze kuonekana; na

(d) Sifa ya wale wanafunzi watakaochukua mafunzo yale pia vyeti vyao vieleweke kabla ya kuanza masomo.

Kwa hivyo, hizo ndizo sifa zinazotakiwa kwa ajili ya kuanzisha chuo hicho *(Makofi)*.

**Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii:** Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kidogo bora nieleze bayana mambo haya *(Makofi)*.

Kwa kweli Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii hatukipingi hiki chuo. Kwa hivyo, tunachokipinga hatutaki Wazanzibari wageuzwe wanyama kwa kufanya majaribio ya matibabu. Kwa hivyo, barua aliyoandikiwa Mkurugenzi wa *Zanzibar Commercial Institute* ya tarehe 14 Mei, inasema hivi:-

Mhe. Spika, baada ya Baraza la Wauguzi na Wakunga kwa kushirikiana na Afisi ya Mafunzo Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii Zanzibar yamegunduliwa mambo yafuatayo:-

(i) Chuo hakina walimu wa kudumu na wengi wanaofundisha si walimu wanaotambulika na Baraza;

(ii) Aliomba kusomesha *PHNB2* na hivi sasa amekuwa akifundisha wauguzi kinyume na maombi yake ya awali, hadi Baraza limekuja kufanya ukaguzi halina taarifa ya kada nyengine inayofundishwa ngazi ya stashahada;

(iii) Kutokana na taarifa ya Mkuu wa Chuo hicho ni kuwa mtaala unaofundishiwa ni mmoja wa kada zote mbili ya *PHNB* na Wauguzi na wala haupaswi kufundishwa wauguzi, kwani mtaala mmoja wanafundishwa Wauguzi na *PHNB*;

(iv) Chuo hakina walimu wa kudumu, mwalimu mmoja yupo ambaye amejitambulisha kuwa ni mwalimu wa kudumu, yaani *full time teacher* ni mwalimu wa Chuo cha Afya Mbweni. Vile vile walimu wanaofundisha kwa *part time* hawajasomea ualimu. Hivyo, walimu ambao wapo ni chini ya kiwango kinachohitajika kuendesha mafunzo haya ya Wauguzi;

(v) Chuo hakina maktaba wala vitabu na viliopo ni vichache kulingana na idadi ya wanafunzi wenyewe;

(vi) Vifaa viliopo kwenye chumba cha mazoezi ni kidogo na vifaa vingi muhimu vimekosekana;

(vii) Madarasa yaliopo ni madogo kulinganisha na idadi kubwa ya wanafunzi waliopo;

(viii) Idadi ya wanafunzi ni kubwa kulingana na mazingira ya kufundisha hususan mafunzo ya vitendo, vifaa vya mazoezi pamoja na wasimamizi wa vitendo katika hospitali zetu; na

(ix) Baraza la Wauguzi linawatilia mashaka ajira ya wahitimu wa *PHNB*, ambao wamechukuliwa kwa wingi na kwa vile hivi sasa mahitaji ya kada hiyo ni ndogo hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, kutokana na hayo Baraza halitambui mafunzo yanayoendeshwa na chuo hicho. Vile vile hawatowatambua wahitimu wa chuo hicho kwa kuwapatia usajili baada ya kuhitimu mafunzo hayo. Kwa hivyo, chuo kinakwenda kinyume na utaratibu na wala hakifuati masharti yoyote na hatujui kinaendesha vipi na kwa hapa Unguja hajakuwa tayari kukaguliwa, yaani hataki kukaguliwa.

**Mhe. Najma Khalfan Juma:** Ahsante sana Mhe. Spika na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa jambo lolote linalotaka kufanya hapa Zanzibar. Kwa mfano, kufunguliwa skuli ya kawaida au chochote huwa inakaguliwa kwanza kwamba skuli hii inao uwezo, inayo madarasa ya kutosha, vitabu vya kutosha pamoja na walimu wa kutosha, ndipo skuli hiyo ifunguliwe. Kwa hivyo, sawa sawa na Chuo cha Afya hakiwezi kufunguliwa mpaka wakaguzi wakikague kabla hakijaanza kazi yake na bila ya kupewa usajili lazima kikaguliwe.

(a) Ilikuwaje kufunguliwa kabla ya ukaguzi wakati hakuna walimu pamoja na vifaa vya kutosha. Hivi sasa wanafunzi wameshaingia gharama ya kulipa na wanasomeshwa na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, inasema haikitambuli chuo hiki?

(b) Wanafunzi hawa wanaosoma hivi sasa na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii haikitambui hiki chuo. Kwa nini hadi hii leo kinaachiwa kuendelea kusomesha na wala hakijafungwa kinasubiri nini mpaka hapo watakapokamilisha hayo matakwa ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii?

**Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii:** Mhe. Spika, baada ya Mkuu wa Chuo kuleta maombi yake, aliambiwa haya yafuatayo:-

(i) Kuwasilisha wizarani taarifa za walimu wake, vifaa na jengo litakalotumika;

(ii) Kutoanzisha masomo mpaka skuli ikaguliwe na kuidhinishwa;

(iii) Mitaala ya mafunzo atakayosomesha; na

(iv) Wanafunzi wawe na sifa sio kuchukua tu barabarani.

Kwa hivyo, alileta mitaala yake na baadaye tunasikia tu chuo kimefunguliwa Unguja na Pemba watu wametangaziwa, yaani anaendesha kiholela na hii ni hatari kwa sababu baadaye hawa wauguzi watakuja kuwashughulikia wananchi yaani wagonjwa, watu waliokuwa hawana taaluma utampa vipi mwili wa mwanadam si anakwenda kumuua huyo, *Yaarabi*.

Sasa tuna nguvu gani? Mwenyewe anaendesha na skuli zimejaa tele. Kwa kweli Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, mambo ya kufungua skuli na kusomesha si juu yetu na anachokisomesha sisi hatukijui na wizara husika ya elimu ipo.

Kwa hivyo, hatujui anachokisomesha kwa sababu Unguja anasomesha na akiambiwa akaguliwe hataki. Sasa ruhusa hiyo kampa nani ya kusomesha.

Mhe. Spika, tunasema na wala hatufichi kwamba chuo hatukitambui kama yeye anasomesha tunamuachia asomeshe na watakapomaliza hatutowapa usajili, kwa sababu wanaotoa usajili ni Baraza la Wauguzi na tayari wao wameshasema kwamba hawatotoa usajili kwa watu wale.

Kwa hivyo, hatujui wanachokifanya, isipokuwa yeye anaendeleza na wenyewe wanafunzi wanatajua hatua za kufanya kama watakwenda kwenye chombo cha sheria na waende.

**Nam. 7**

**Mfumo wa Usafirishaji wa Fedha wa *TISS***

**Mhe. Fatma Abdalla Tamim (Kny: Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi)** Aliuliza:-

Mfumo wa usafirishaji fedha wa *TISS* ni salama na unarahisisha usafirishaji wa fedha.

(a) Mhe. Waziri, jee, Benki ya Watu wa Zanzibar (*PBZ*) inatumia mfumo huu?

(b) Kama inatumia mfumo huo benki imepata mafanikio gani tangu ianze kutumia mfumo huo?

(c) Zaidi ya mfumo huo *PBZ* inatumia mfumo gani mwingine wa usafirishaji wa fedha ulio salama na haraka?

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi –** Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 7 (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

*Tanzania Interbank Settlement System* (*TISS)* ni mfumo wa malipo ya papo kwa papo unaoendeshwa na Benki Kuu ya Tanzania. Mfumo huu ulianzishwa mnamo April 18, 2004 ukiwa na lengo kuu la kuboresha zaidi, pia kurahisisha njia za kutuma na kupokea malipo ya papo kwa papo kupitia mtandao wa kompyuta, mfumo hujulikana kwa kitaalamu kama "*Real Time Gross Settlement*" (*RTGS*).

a) Benki ya Watu wa Zanzibar ilijiunga na mfumo huu mara tu ulipoanzishwa mwaka 2004,

b) Mafanikio ambayo Benki ya Watu wa Zanzibar imeyapata kutokana na kujiunga na mfumo huu ni haya yafuatayo:-

   i) Mfumo huu unachochea maendeleo ya shughuli za kiuchumi kwa kurahisisha na kuharakisha malipo mbali mbali ya wateja wa Benki ya Watu wa Zanzibar;

   ii) Kurahisisha upelekaji na upatikanaji wa malipo kwa wateja wa Benki ya Watu wa Zanzibar, yanayokwenda na yatokayo benki nyengine. Hii ni pamoja na malipo ya kodi ya *TRA* na *ZRB*;

   iii) Mfumo huu umeweza kupunguza kwa kiasi kikubwa wizi na ghushi zitokanazo na usafirishaji wa fedha nchini, hivyo kuimarisha usalama wa malipo mbali mbali yafanywa kupitia mfumo huu;

iv) Wateja umepunguziwa gharama za usafirishaji fedha kutoka benki moja kwenda benki nyingine, gharama za *TISS* kwa muamala (*transaction*) mmoja hivi sasa ni shiligni 10,000/-; na

v) Benki ya Watu wa Zanzibar imefanikiwa kuzifanya huduma zake kwa wateja kuwa bora zaidi, pia kupunguza malalamiko yatokanayo na ucheleweshaji wa kusafirisha fedha.

c) *PBZ* inayo mifumo mingine salama ya kusafirisha fedha nje ya nchi ambayo ni pamoja na ifuatayo:-

i) *Society for World Interbank Financial Telecommunication* (*SWIFT)*. Huu ni mtandao wa kompyuta unaomilikiwa na mabenki duniani. *PBZ* ilijiunga nma Mtandao huu mwka 2003. *SWIFT* inawezesha *PBZ* kutuma fedha kwa usalama na haraka popote ulimwenguni; na

ii) Citidirect. Huu ni mfumo wa kutuma fedha kwenda nje ya nchi kupitia Benki ya Citi iliyopo New York Marekani. Mfumo huuu huiwezesha *PBZ* kutuma fedha za sarafu za Dola za Kimarekani kwa haraka pale mfumo wa *SWIFT* unapopata matatizo. Kwa kifupi mfumo wa *Citidirect* unaegemea kwenye huduma ya *Interbanking*.

**Mhe. Said Ali Mbarouk:** Nakushukuru Mhe. Spika, naomba nimuulize Mhe. Waziri kwamba ninayo habari kwamba Benki Kuu ya Tanzania (*BoT*), imeishauri Bodi ya Mapato Zanzibar (*ZRB*) kutumia mfumo huu wa *TISS* katika ukusanyaji wa mapato na usafirishaji wake, ili kuvuia mianya ya upotevu wa fedha.

Lakini *ZRB* ikawa na wasi wasi au kutokubali na mfumo huu wa *TISS*. Je, habari hii ni kweli Mhe. Waziri na kama ni kweli ni sababu ipi iliyowafanya *ZRB* kukataa ushauri huo wa kitaalamu wa *BoT*?

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi:** Mhe. Spika, si kwamba *ZRB* wamekataa isipokuwa hatua iliopo ni kufanya utafiti wa njia mbali mbali za kulipa mapato *ZRB* na si lazima kwa huu wa *SWIFT* tu.

Lakini kwa njia nyengine zaidi ya fedha mkononi kama inavyofanywa au kwa njia ya hundi.

Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Mjumbe kwa upande mmoja kwamba *ZRB* wanafanya tafiti kwa njia nyengine za kulipwa. Kwa hivyo, kuhusu *BoT* wamewashauri na kukataa si kweli. Jambo liliopo ni kwamba wanafanya utafiti kwa njia mbadala za kuwalipa kodi zao.

**Nam. 71**

**Ajali ya Kuungua Moto M.V Serengeti**

**Mhe. Hija Hassan Hija –** Aliuliza:-

Miezi michache nyuma meli ya M.V Serengeti inayomilikiwa na Kampuni ya *JAK ENTERPRISES L.T.D* ilipata ajali ya kuungua na moto wakati ikiwa nangani Bandarini Zanzibar.

Tukio hilo liliongeza hofu kwa Wazanzibari na wasafiri wengine, kwani baada ya M.V Mapinduzi na M.V Maendeleo kushindwa kufanyakazi na kutoa huduma za usafiri, M.V Serengeti ndiyo iliyokuwa mkombozi kwa sekta ya usafiri wa baharini.

(a) Mhe. Waziri nini chanzo cha ajali hiyo?

(b) Je, Kampuni inayomiliki meli hiyo iliingia hasara kiasi gani?

(c) Zipo taarifa kuwa Kampuni ya *JAK* imeamua kuitengeneza meli hiyo pale pale ilipo badala ya kuipeleka Chelezoni Mombasa. Je, suala hilo ni kweli?

(d) Kama ni kweli na upo uwezekano wa kuifanyia matengenezo meli hiyo, ni kwa nini meli zetu hasa M.V Maendeleo tusiifanyie matengenezo hapa hapa ili kuokoa fedha?

**Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi -** Alijibu**:-**

Mhe. Spika, awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa wazima na kuhudhuria kikao cha Baraza, kwa ajili ya kutekeleza majukumu yetu tuliyopangiwa.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nambari 71 (a), (b), (c) na (d) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 71 naomba kutoa maelezo yafuatayo. Ni kweli kwamba mnamo tarehe 13/3/2010 meli ya

M.V Serengeti ilipata ajali ya kuungua moto wakati ikiwa nangani. Meli hii ilikuwa kiungo muhimu sana kwa usafiri baina ya Unguja na Pemba, hususan kutokana na ratiba yake ya kuaminika na idadi ya watu inayopakia.

Hata hivyo hali ya usafiri kwa sasa baina ya Unguja na Pemba inaendelea vizuri, kwani kuna boti za kasi kila siku isipokuwa siku za Jumapili na Ijumaa. Kwa hivyo, Boti ya *Seagull* imechukua ratiba ya Serengeti na Meli ya Buraq inakwenda Jumapili na Jumatano.

Mhe. Spika, napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza sana wamiliki wa *Seagull* na *Buraq* kwa moyo wao wa kizalendo kwa kuamua kutoa huduma ya safari za Pemba baada ya Serengeti kuungua.

Baada ya maelezo hayo naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 71 lenye vifungu (a), (b), (c) na (d)

(a) Meli hiyo ilikuwa iko nangani ikifanya kazi ya kuchomea (*welding)* katika deki ya chini. Wakati kazi hiyo ikiendelea joto kali lilipenya katika bomba linalopitisha waya kuelekea sehemu za juu za *saloon*, yaani sehemu ya abiria, ambapo joto hilo liliweza kuunguza vitu vinavyoshika moto kwa urahisi. Hivyo kuifanya meli hiyo kuungua kwa haraka, kwani eneo hilo la abiria lina viti na vitu vyengine, ambavyo vinawaka kwa haraka;

(b) Kutokana na ajali hiyo ya moto kampuni inayomiliki meli hiyo imeingia hasara ya kiasi cha dola laki sita; na

(c) Ni kweli kuwa kampuni ya *JAK* imemleta mtaalamu wa kuiunda upya meli hiyo sehemu zilizoungua na kuirudisha kama ilivyokuwa zamani, badala ya kuipeleka meli hiyo Chelezoni Mombasa

Hii inatokana na kupunguza uwezekano wa kukaa Chelezoni kwa muda mrefu. Hata hivyo, meli hiyo sasa inajiandaa kwenda Chelezoni Mombasa, kwa ajili ya kufanyiwa matengenezo sehemu ya mkuku.

Vile vile meli zetu pia za M.V Maendeleo na Ukombozi huanza kufanya matengenezo hapa, kwa ajili ya kupunguza muda wa kukaa Chelezoni Mombasa.

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Spika, baada ya majibu ya Mhe. Naibu Waziri naomba nimuulize swali moja la nyongeza lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Waziri amekiri kwamba sababu kubwa ya meli hiyo kuungua ni kwamba walikuwa wakichomea wakati wakiwa nangani. Lakini nakumbuka siku ile ilikuwa ni siku ya safari na mimi nilikuwa abiria mmoja.

(a) Je, ni utaratibu wa meli kutengenezwa wakati meli hiyo iko kwenye safari au utaratibu ni kupeleka Chelezoni ikiwa na matatizo?

(b) Kampuni imeingia hasara ya dola laki sita, je serikali imesaidia kiasi gani?

(c) Kampuni ya *JAK* ilikuwa na lengo la kutengeneza meli ile hapa Zanzibar bila ya kuipeleka Mombasa. Lakini taarifa zilizopo kwamba ikiwa meli ile wataitengeneza hapa Zanzibar, basi baadaye haitokuwa na ruhusa ya kufanyakazi Zanzibar. Je, hilo ni kweli?

**Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi:** Mhe. Spika,

a) Kwanza kabisa Mhe. Hijja Hassan kauliza kwamba utaratibu wa kutengenezwa meli katika siku ya safari je suala la kawaida;

Mhe. Spika, matengenezo madogo unaweza kuyafanya pengine katika utaratibu huo lakini kama matengenezo ni makubwa maana yake lazima itabidi uahirishe safari kwa sababu unaweza kuchelewa au kusababisha tatizo ambalo kama ilivyotokea;

b) Serikali pengine kusaidia kiasi gani. Mhe. Spika, meli hii kama zilivyo meli nyengine zinakuwa na bima kwa hivyo inaptokea tatizo moja kwa moja bima ndio inawajibika kuwalipa na sio serikali; na

c) Kampuni ya *JET* lengo lake ni kuitengeneza meli ikiwa hapa hapa Zanzibar, lakini wamelazimika kwenda Mombasa baada ya kupewa shinikizo na serikali kwamba ikiwa meli hii haitakwenda Mombasa baadaye haitapewa leseni ya kufanya kazi hapa Zanzibar. Je hilo ni kweli?

Mhe. Spika, mbali ya meli hii ya Serengeti meli zote ambazo zinafanya matengenezo, kuna matengenezo ambayo tunaweza kuyafanya hapa nchini lakini kuna baadhi ya matengenezo lazima ipelekwe Mombasa kutokana ukubwa wa matengenezo hayo ambapo sisi hatuna uwezo nayo. Kwa hivyo na wao vile vile baada ya kumalizika matengenezo madogo watalazimika lazima waipeleke kule kwa sababu ile sehemu ya Mkuku lazima ipandishwe juu na iweze kufanyiwa matengenezo ambayo yanahusika.

**Mhe. Hamad Masoud Hamad:** Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Spika, wakati Serengeti ilipopata ajali ya kuungua wamiliki walilia sana lakini wasafiri baina ya Unguja na Pemba walilia mara mbili, ni meli pekee hadi sasa inayokwenda na wasafiri wakiwa na mizigo ya aina yoyote paka, kuku, ndizi.

Hizo *Speed* boti nyengine hakuna fursa kama hii, sasa kwa mwekezaji kama huyu na wengine kama hawa wanaopata ajali kama hii Je, kuna utaratibu wowote wa serikali, au vivutio vyovyote vya serikali maalum isiyokuwa bima ambayo serikali imeweka kwa ajili ya wanaopata hasara kama hizi na ni wawekezaji maalum hasa kwa visiwa vya Unguja na Pemba?

**Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi:** Kwanza kwa sababu Mhe. Hamad Masoud Hamad ni mjumbe wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ni mmoja katika wadau wazuri katika Wizara yetu, lakini hata hivyo naomba akumbuke tu kwamba kiutaratibu wa serikali hakuna utaratibu huo popote pale duniani. Isipokuwa kukiwa na matatizo ambayo serikali tuna uwezo nayo yaani yako ndani ya uwezo wetu basi tunawajibika kuwasaidia wenzetu.

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi:** Mhe. Spika, tuna utaratibu kwa mradi wowote ambao umeandikishwa *ZIPA* basi tunawapa vivutio kama ni mradi wa uwekezaji. Kwa hivyo miradi kama hii yote ya usafirishaji maboti mapya haya wakija na wameandikwa *ZIPA* tunawapa *Tax holiday* kwanza miaka mitatu kama taratibu za *ZIPA* zinavyosema.

Pili wanapoagiza vifaa basi vile vifaa pia tunawasamehe kodi ili mradi ule ujiendeleze nasisitiza kama mradi umepitia *ZIPA.*

**Mhe. Subeit Khamis Faki:** Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa sababu meli ya MV. Serengeti ilipata ajali ya kuungua na kwa kuwa chombo chochote kile kikiwa kimekata bima kinapopata ajali kinakuwa kinalipwa na bima. Je, meli ya MV. Serengeti matengenezo yote hayo yanayotengenezwa kuanzia hapa mpaka kupelekwa chelezoni. Je, matengenezo hayo yanasimamiwa na bima.

**Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi:** Kama nilivyojibu suala langu la msingi ni kwamba chombo chochote ambacho kina bima kinapopata ajali basi bima ina wajibu wa kuwalipa moja kwa moja, sasa aidha Serengeti wamelipwa na bima au laa inategemea kwamba walikuwa na bima au laa.

## HOJA ZA SERIKALI

*(Majadiliano yanaendelea)*

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011

**Mhe. Hamad Masoud Hamad:** Mhe. Spika, nakushukuru tena kwa mara ya pili leo asubuhi hii kunipa nafasi ya kuendelea kuchangia mswada huu wa hotuba ya Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Katiba na Utawala Bora, katika kujadili bajeti ya Wizara yake ya mwaka 2010/2011.

Kwa hivyo sitaki kujibu ambayo wenzangu wamesema lakini suala la mswada wa haki za watoto ambalo jana lilizungumzwa kama wenzangu waliotangulia ni mswada ambao umewatia mashaka makubwa walioko nje ya Baraza hili. Ndio maana Misikiti sio mmoja tu ni mingi sana katika hotuba zao hili huwa linazungumzwa sana.

Kwa kweli ni ajenda au *current issue* kwa siku hizi mwenzangu alitangulia kusema akasema hii ni dhana na akatoa aya. Hii sio dhana mswada upo na katika mswada huu, hao Mashehe ambao wanahutubia wana–*quote* na vifungu, kwa hivyo sio suala la kwamba halijafika hapa ni dhana au halipo mimi nasema lipo.

Moja katika mfano na kifungu kilichosomwa ni kwamba endapo mzazi atampiga bakora mwanawe basi ikithibiti hivyo mzazi huyo ana kifungo cha miaka kumi na tano. Sasa hili lazima Mashehe walizungumze hulka na silka zetu sisi tusingesoma chuoni bila ya bakora. Wengine hawaendi skuli wanatoroka ukiwapiga bakora wanakwenda skuli mpaka wanamaliza vyuo.

Wanaposema mambo haya hawasemi kubahatisha, mimi sheria hiyo ikija hapa siku hiyo nitatoka kabisa siichangii hilo. Nataka kulikumbusha kwamba huo

mswada upo hata Maalim Mohamed Ali Salim anayo *draft* kama mjumbe wa Kamati, wadau wameshaitwa kama hao Mashehe na ndio maana ni gumzo ukija hapa mimi nasema ni miongoni mwa watakaotoroka hapa.

Pili Mhe. Spika, Tume ya Kuchunguza Sheria kwa kweli tume hii ipo siku nyingi na ni wajibu wa serikali yoyote kuwa na tume kama hii, kwa sababu dunia inakwenda na wakati. Kuna sheria nyingi za kikoloni ambazo tumezifuta na nyengine bado zipo. Kwa hivyo umuhimu wa tume hii kwa serikali yoyote na hasa kwa nchi ambayo ina utawala bora ina umuhimu wake. Lakini sasa ni kwa nini hadi sasa hakuna Mwenyekiti na Makamishna wa tume hii, Waziri aje atuambie ni kwa nini.

Sasa hivi Zanzibar ina wimbi la wanasheria, tuna zaidi ya wahitimu kila mwaka kutoka chuo cha Tunguu, Dar es Salaam *University, Mzumbe* na vyuo vyengine. Wazanzibari ambao wako hapa wengine hata kazi hawana, sasa tukiambiwa kwamba mpaka leo Makamishna na Mwenyekiti wa Tume hii muhimu hawapo tunashindwa kuelewa. Lakini sio hilo tu, hapa sio kwamba tume haina Mwenyekiti na Kamishna lakini ina wafanyakazi wangapi kwa sababu kwa mwaka 2009/2010, Waziri anatuambia katika kitabu chake mishahara na maposho ilikuwa ni Shs.146,731,000 kama Tume haina hata Mwenyekiti na Makamishna ni kazi gani inafanywa na Tume hii kwa fedha nyingi kiasi hiki.

Mhe. Spika, Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka hii Afisi ina miaka minane tu lakini umri huu wa miaka minane kwa mafanikio yake unaweza kusema ina umri wa miaka thamanini ile nane ukaongeza zero kule mbele. Kuna taasisi kama hizi zina miaka kumi mpaka kumi na tano au ishirini hazijafika hata nusu ya utendaji na ufanisi wa afisi hii. Tujiulize kulikoni, mimi hapa nashauri kabisa kwa sababu inawezekana na ushahidi ni huu, viongozi wa taasisi hizi wawe wabunifu, waige kama inawezekana kwa afisi hii, isiwezekane kwa nini, kwa afisi kama hii ya Mwanasheria Mkuu.

Mapungufu yaliyokuwepo kwa Mwanasheria Mkuu ni makubwa tukiyasema hapa tutafika kesho na bahati mbaya muda hauturuhusu. Kwa hivyo mimi natoa wito na nashauri kabisa sio kusema kwa Mwanasheria Mkuu tu lakini hata taasisi nyengine ziige ubunifu, kuiga ni jambo zuri sio vibaya na ndio maana watu wanaendelea kwa sababu hiyo. Afisi hii kuna siri gani wakae na Mkurugenzi hata kama ni semina waelekezane. Kuna hiki na hiki na njia hii mimi nimepita ili na wao wapite afisi zetu zote zing'are kama hii.

Mhe. Spika, ufanisi mkubwa ambao unaonekana wazi wazi tangu ofisi hii ianzishwe na kuanza kufanya kazi zake ni ule utaratibu wa kuwa na PP ambaye ni polisi umeondoka. Mimi nilikuwa wakati mmoja Mkurugenzi wa haki za

binadamu katika chama changu cha CUF, uzoefu wakati ule ambapo afisi hii ilikuwa haijaanza kazi zake au pengine hata kuanzishwa huwezi kusema, yaani askari kama *PP* walikuwa wananyanyasa watu kupita kiasi na siku zile siasa ndio imekaza. Lakini Mhe. Spika, pamoja na kwamba bado siasa ipo ni kipindi kirefu sasa hivi tangu afisi hii ianzishwe na hawa waendesha mashitaka kuwa sio polisi tena. Kwa kweli tumepata unafuu mkubwa, unaona kabisa wazi wazi kwamba haki inatendeka.

Nahimiza kwamba kwa zile wilaya ambazo hazijapata waendesha mashitaka ambao sio polis,i basi afisi hii iharikishe ili tuwe na *uniformity* si vizuri kwamba Afisi ya Mwanakwerekwe kuna mwendesha mashitaka ambaye sio polisi. Lakini afisi pengine ya Mkokotoni hakuna fursa kama hiyo na bado pengine watu wanaendelea kunyanyaswa na *PP* ambaye ni polisi. Hii itajenga imani kwa wananchi kwamba kweli sasa Mahakama zinatoa haki, lakini kama zitakuwa zinatoa haki ni sifa kwa serikali na sisi ndio tuna utawala bora. Kwa hivyo hii ni kusaidia tu katika kuimarisha utawala bora katika sekta zote kwenye mashtaka ambako ni Mahakama na kwengineko.

Mhe. Spika, wizara hii ni mtambuka kila pahali ipo lakini ina utawala bora. Juzi tulipokuwa tunajadili hotuba ya Mhe. Waziri Kiongozi katika mambo ya Tume ya Uchaguzi huu mfano wa karatasi ya kura ya maoni ilikuwa haujatoka. Lakini kwa bahati nzuri karatasi hii ninayo imeanza kusambazwa na sisi rasmi tumepewa hapa ndio nilizokuwa nazo mimi hapa.

Hii ni ya Tume ya Uchaguzi lakini nasema kwamba utawala bora uko kila mahali, kwa hivyo kwa sababu hii ilikuwa haijapatikana haikuweza kusemewa pale.

Naomba niisemee hapa. Sheria hii tuliipitisha hapa na tukasema hasa kwamba masuala katika kura ya maoni yawe *specific* ili upate *specific answer,* sasa hii wanasema ni mfano, Tume ya Uchaugizi ya Zanzibar karatasi ya kupiga kura ya maoni tarehe 31 Julai, 2010.

Suala linasema hivi je, unakubali kuwepo kwa muundo mpya wa serikali mara baada ya uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010. Hilo ndilo swali, sasa hili swali sio *specific* linakanganya sawa sawa na kumuuliza Mhe. Naibu Waziri Kiongozi hapo, Mheshimiwa utakwenda useme ndio au hapana.

Lazima akuulize tana wapi lakini ukimwambia Mheshimiwa tunasali Msikiti wa Ijumaa hapa leo jee, utakwenda kusali hapa, hakuulizi tena atakwambia nitakwenda au siendi. Sasa hili swali nasema haliko *specific* na hili huwezi kupata jibu sahihi litakanganya watu sana, chini ya hapo kuna kisanduku ndiyo kushoto na hapana kulia.

Mimi napendekeza kwamba ili mtu usimkanganye na asighumiwe, asiwe na wasi wasi awe na uhakika anachokitaka basi suala liwe hivi. Je, unakubali kuwepo kwa huu muundo mpya. Je, unakubali kuwepo kwa serikali ya umoja wa kitaifa mara baada ya uchaguzi mkuu 2010 nasema hayo ni mapendekezo yangu, labda karatasi hii imesambazwa kwa maoni ya watu. Naona ombi hili langu mimi Mhe. Waziri kama alivyosema hii ni Tume ya Uchaguzi lakini utawala bora upo kila pahali ni *cross country,* kwa hivyo hii naomba uiwasilishe kwa sababu watu wa tume ya uchaguzi hapa hawapo.

Mhe. Spika, Mahakama jamani ni mhimili wa pili wa uongozi wa nchi, si kwa maana ya nambari aah! mihimili ni mitatu Baraza la Wawakilishi au chombo cha kutunga sheria ni moja, Mahakama na serikali kwa maana ya Rais na watendaji wake. Sasa Mahakama zetu siku zote zinapigiwa kelele katika Baraza hili, bado hazijakuwa Mahakama zenye *standard* inayotakiwa. Hiyo *standard* huipati kama huna watu wenye elimu. Zamani mara baada ya mapinduzi kulikuwa na Mahakama za wananchi na mimi siku hizo mdogo lakini nilikuwa nahadithiwa kwamba ilikuwa kesi inasemwa wee! Jaji aliyekuweko pale koti lake ukitwikwa unaweza kuanguka.

Lakini mkishasema saa mwengine anasinzia anakwambia chungulia chini, baba watu wanapita hivi anakwambia wote wale hawakuletwa hapa kwa sababu hawana makosa, wewe una kosa unakwenda miaka kumi au kumi na tano utaratibu ule umeondoka kwa sababu gani. Kwa sababu watu wameanza kujifunza bado Mahakama inatakiwa iwe na wataalamu wa kutosha. Wenzetu Bara kila siku unasikia hapa, Mahakama Kuu Rais Kikwete kawateua kumi au kumi na tano anawaapisha, yaani unahisi kwamba kweli kuna *movement*. Sasa huwezi kupata wataalamu kama huwasomeshi.

Mhe. Spika, *item party two* inasema hivi vichekesho, Mahakimu wa ngazi mbali mbali walishiriki katika semina ya kuwajengea uwezo juu ya sheria ya uvuvi mwaka mzima huo, semina hiyo ilitayarishwa na Idara ya Uvuvi Zanzibar kwa kushirikiana na Mahakama kwa semina moja. Makarani wa Unguja na Pemba nao wameshiriki katika semina iliyotayarishwa na kituo cha huduma za sheria Zanzibar ili kuwajengea uwezo juu ya sheria zao za kila siku, mahakama nyengine hizi semina ndio mafunzo ni uzoefu. Semina maana yake ni *practical experience* mnakuja kupewa, sasa mwaka mzima Mahakimu wa Unguja na Pemba wanafanya semina moja sheria ya uvuvi, makarani wa Unguja na Pemba wanafanya hivyo, hivi ni vichekesho mimi nimeweka makusudi hapa.

Mhe. Waziri sisi tu hapa Baraza la Wawakilishi kwa sababu ya ubunifu wa watendaji wa hapa tumefanya semina mpaka nyengine unajua hasa kwamba kweli Baraza la Wawakilishi sasa hivi limekubali kuji-*transform* Spika, hata

kama siku ya Jumamosi anakwambia lete semina wanatafuta sehemu mbali mbali, mabenki, Bima na sehemu mbali mbali tunaelimishwa unajua sasa hapa Baraza madhubuti. Sasa kusema semina moja kwa mwaka ni aibu.

**Mhe. Spika:** Katika mkutano huu ipo moja kubwa.

**Mhe. Hamad Masoud Hamad:** Haya taarifa hizo katika mkutano huu ipo semina nyengine moja na posho ni lile lile.

Mhe. Spika, Mahakamani anapopelekwa mshitakiwa wana sheria zao ambazo hatuzipingi kabisa, lakini inapokuja wakati wa dhamana tujue kwamba dhamani ni haki ya mshtakiwa, wanavyo vifungu vyao mimi nazungumzia si suala kwamba watu wapewe dhamana au wasipewe, lakini ninachozungumzia hapa Mhe. Spika, ni kwamba umeshtakiwa kwa kosa ambalo hukumu yake hata ikithibiti ni ndogo kuliko ile dhamana unayoambiwa utoe.

Mfano umeshitakiwa kwa kosa la uzembe na uzururaji, maana yake ipo hiyo pengine hukumu yake ikithibiti ni shilingi laki moja lakini unaambiwa dhamana hapa shilingi milioni mbili, hiyo ni hakika kwamba hakimu kwa sababu ana uwezo huo anataka kumkomoa mtu, lakini twende mbali zaidi hata hizo milioni mbili zikitolewa kama dhamana kesi ile inapokwisha inakuwa ni papatu kurudishiwa dhamana yako. Kesi imekwisha na umeshinda kuzipata ile dhamana uliyotoa ni papatu bwana hawana uharaka kama ule wa wao kuwapa dhamana, wao wanachukua muda mrefu pesa zimekopwa mpaka wengine wanakimbia nchi, Mahakama haijataka kutoa pesa ambazo zilimdhamini aliyekukopesha haondoki kwako inabidi sasa utoroke.

Sasa nasema haki isiangaliwe kwa upande mmoja iangaliwe kwa pande zote hukumu ya kesi na dhamana lakini na pesa ambazo zinachukuliwa kama dhamana zirejeshwe baada ya kesi kumalizika.

**Mhe. Spika:** Mheshimiwa jali muda.

Mhe. Spika, la mwisho ni jumuiya zilizoombewa msaada na msamaha wa ushuru ni kwa ajili ya shughuli gani jumuiya hizi wameombewa msamaha wa ushuru na jee wamepatiwa msamaha huo, kama wasingepatiwa kungekuwa na athari gani kwa taasisi zao, ni nani aliyewaombea msamaha huu wa ushuru nakusudia hapa ni Wizara au Afisi ya Mufti niambiwe ni nani hasa ambaye aliwaombea. Serikali imethibitisha vipi Mhe. Salmin Awadh alizungumzia jana hili kwa Halmashauri lakini nasema serikali imethibitisha vipi kwamba msamaha uliosamehewa kweli unatumika kwa madhumuni iliyoombewa au kuna mambo tu yanafanyika.

Mhe. Spika, umenipa dakika mbili sitaki nizimalize kabisa lakini la mwisho kabisa ni uajiri katika Mahakama kuu. Hii ina tume yake ya utumishi lakini juzi kwenye vyombo vya habari nilisikia kwamba kuna upungufu wa majaji wa Mahakama Kuu. Mimi nasema ni sawa lakini ninachosisitiza hapa ni kwamba kuna wanasheria wako kwa *state attorney* wengi tu wana uzoefu ya muda mrefu miaka zaidi ya kumi mpaka kumi na tano. Jaji wa Mahakama Kuu anaweza kabisa kutoka katika Afisi ya Mwanasheria Mkuu imeshatendeka naomba nimtaje Mhe. Makamo Mwenyekiti wa Tume ya uchaguzi Bara Mhe. Makungu alitoka kwenye Afisi ya Mwanasheria Mkuu na moja kwa moja akateuliwa kuwa Jaji wa Mahakama Kuu.

Sasa kwa sababu kuna wengi wenye uzoefu huo nashauri sana tume ya uajiri kabla haijatafuta kutoka Bara au kutafuta mtu wa hapa hapa ambaye ana uzoefu mdogo pengine wa miaka sita, hata kama alikuwa Hakimu lakini watu wenye uzoefu wa miaka kumi, kumi na tano katika afisi ya Mwanasheria Mkuu wa kuendesha kesi kubwa kubwa wapo, keshokutwa tunaweza kusikia kwamba fulani kateuliwa kuwa Jaji wa Mahakama Kuu ukimchunguza pengine ni Hakimu aliye na uzoefu wa miaka sita, lakini wale wenye uzoefu wa zaidi ya miaka kumi na tano wameachwa hii inaleta sura mbaya na inaleta tafsiri mbaya katika Mahakama kitu ambacho kinatakiwa kiwe mfano katika kuleta uadilifu.

Mhe. Spika, kwa haya machache nakushukuru sana. Ahsante. *(Makofi)*

**Mhe. Salmin Awadh Salmin:** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii na mimi nikaeleza kwa muhtasari tu kuchangia mawili matatu juu ya hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia siku hii ya leo kuweza kufika hapa katika Baraza lako tukufu kwa ajili ya shughuli zetu hizi za kawaida za kila siku.

Mhe. Spika, kwanza nitumie nafasi hii kumpongeza Mhe. Waziri Ramadhani Abdalla Shaaban kwa hotuba yake hii nzuri, imepangika imegusa karibu maeneo yote tunampongeza, tunawapongeza watendaji wake, Katibu Mkuu wa Wizara pamoja na Wakurugenzi na maofisa mbali mbali wa wizara hii kwa kazi kubwa, nzuri na nzito ambayo wanaifanya kila siku.

Mhe. Spika, tutumie pia nafasi hii kumpongeza kwa dhati kabisa Mhe. Waziri wa Wizara hii kwa kulizungumzia suala lile ambalo mara nyingi tumekuwa tukilizungumza hapa tokea tuingie. Suala la utafutaji na uchimbaji wa mafuta. Kwa hivyo tunakupongeza *at least* Mhe. Waziri hili umeliona kwamba halijaguswa wala halijazungumzwa na hatuna matumaini ya mtu mwengine kulizungumza.

Lakini katika hotuba yako hii umetuelezea kwamba uamuzi wa Baraza la Wawakilishi kupitisha maamuzi ya kufanya suala la utafiti na uchimbaji wa mafuta na gesi lisiwe suala la muungano uwezekano wa kulifanya suala hili kuwa si suala la muungano ni mkubwa sana. Kwa hivyo hii ni *statement* nzuri na kwa kweli tunakupongeza sana kwa ujasiri wako na uzalendo wako.

Mhe. Spika, Idara hii ya Utawala Bora au Wizara hii ya Utawala Bora kama mwenzangu alivyotangulia ni wizara mtambuka ambayo imekusanya maeneo mengi na zaidi suala zima la utawala bora. Suala la utawala bora limegusa maeneo yote na ndio msingi wa kuendesha nchi. Ni wajibu wa wizara hii kuona imekava maeneo yote katika kuhakikisha kwamba utawala bora unakuwepo visiwani kwetu. Wizara ina kazi kubwa na kutokana na kuwa ina maeneo mengi. Maeneo haya ni lazima wizara ihakikishe inayafanyia kazi ipasavyo.

Leo tukianza kuyazungumzia hata muda wako huu utakuwa hautoshi lakini nitayagusia baadhi tu maeneo ambayo Wizara kwa kutumia nembo hii ya utawala bora inaweza ikaishauri serikali ipasavyo au inaweza ikaushauri Baraza la Mapinduzi ipasavyo ili kuona huu msingi wa utawala bora kwa visiwani kwetu unakuwepo.

Mhe. Spika, nizungumzie suala la mgawanyo wa madaraka kwa mujibu wa Katiba, ibara ya 5 (a) kifungu cha 1, 2 na cha 3. Suala la mgawanyo wa madaraka limekuwa likizungumzwa sana katika chombo hiki. Inaonekana kwamba bado halijaweza kutekelezwa ipasavyo. Mihimili hii mitatu ni muhimu sana kwa sababu ndio mihimili iliyosimamisha serikali. Kwa hivyo kuuachia muhimili mmoja kuwa na nguvu zaidi hii inaonesha dhahiri kwamba hapa utawala bora unapindwa. Kwa sababu mihimili hii inatakiwa iwe na nguvu sawa na iweze kutekeleza majukumu yake bila ya kikwazo.

Kumekuwa na malalamiko juu ya mgawanyo wa raslimali hii katika kuendesha vyombo hivi. Bado inaonekana raslimali hii imeshikiliwa na mamlaka moja. Wakati mwengine hizi mamlaka mbili zinapohitaji matumizi ni lazima ziende kupiga magoti kwa mhimili mmoja ni jambo la hatari.

Hapa utawala bora haupo na utaondoka, kwa sababu unavinyima fursa vyombo vyengine kufanya wajibu wake. Chombo kama Mahakama ambacho kinatakiwa kiwe kinatoa maamuzi ya haki. Chombo kama Baraza la Wawakilishi ambacho ndio kinatakiwa kusimamia serikali. Suala la utawala bora katika eneo hili bado linatutia mashaka. Sijui Wizara yako inalishughulikia vipi jambo hili.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri namuonesha eneo linalohitaji kushughulikiwa. Katika maeneo yanayohitaji kushughulikiwa hasa ni eneo hili. Kukosekana kwa

migawanyo hii ya fedha, maana yake vyombo hivi havifanyi shughuli zake ipasavyo. Kila wakati vinakuwa vikienda kuipigia magoti serikali jambo ambalo si sahihi.

Mhe. Spika, wenzetu Bunge la Jamhuri ya Muungano walikuwa nalo muda mkubwa hili, sasa hivi wameshalitafutia ufumbuzi baada ya kuona athari yake. Ningelimuomba Mhe. Waziri achukue mifano kwa wenzetu ili kuona jambo hili linachukuliwa hatua. Halipendezi kuonekana jambo hili kila wakati linazungumzwa katika chombo hiki, lizungumzwe lakini ifike pahala kuonekane utekelezaji wake kwa sababu tunapolizungumza maana yake tunazungumza kwa misingi. Kwa hivyo ni wajibu wa wizara hii kuona kwamba inalisimamia na kuhakikisha kuona kwamba hapa utawala bora unakuwa hauna kasoro.

Mhe. Spika, jengine ambalo ni eneo la Kikatiba ambalo Mhe. Waziri ningeomba nalo alishughulikie. Mimi nimekuwa likinipa mashaka makubwa. Kwa mujibu wa Katiba yetu hii ya Zanzibar ibara ya 47 inazungumzia nafasi ya Naibu Waziri katika serikali hii. Katiba inasema kwamba naomba Mhe. Spika, ninukuu:-

> Ibara ya 47 "Rais anaweza kwa kushauriana na Waziri Kiongozi kuteuwa Naibu Mawaziri kutoka miongoni mwa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ili kumsaidia Rais, Waziri Kiongozi na Mawaziri katika utekelezaji wa kazi zao na hawataanza kazi zao mpaka kwanza wale kiapo cha uaminifu na kiapo cha utekelezaji wa kazi zao kama vitakavyowekwa na Baraza la Wawakilishi".

Mhe. Spika, *statement* hii iko sawa lakini mbona utekelezaji wake sio sahihi. Manaibu Mawaziri kwa mujibu wa Katiba wameelezwa watakuwa ndio wasaidizi wa Mawaziri. Leo sisi tunashangaa hapa kwamba Waziri anapokuwa hayupo anateuliwa Waziri mwengine kukamata ile nafasi sasa hawa kazi yao nini.

Kuna lugha inaambiwa kwamba Manaibu Mawaziri sio wajumbe wa Baraza la Mapinduzi, lakini kwa nini wasiwe wajumbe wa Baraza la Mapinduzi wakati ndio wasaidizi wa mawaziri.

Wanapokuwa hawapo wao ndio wanatakiwa wachukue nafasi, hapa pana kasoro Mhe. Spika. Kasoro hizi tunaziona wakati wa utekelezaji hasa wakati wa shughuli za kamati analetwa Waziri katika Wizara ambayo sio yake. Matokeo yake anakuwa hana analolijua hata moja katika wizara ile. Hapa

panaonekana pana kasoro kubwa. Wenzetu Tanzania Bara wameshatoka kule, tayari Manaibu Mawaziri wanatumika kama wasaidizi wa mawaziri kwa sababu wao wanakuwa wanaijua fika ile wizara yao ilivyo.

Mhe. Waziri eneo hili linahitaji kufanyiwa kazi. Kama ikibidi Manaibu Mawaziri kuwa Wajumbe wa Baraza la Mapinduzi basi na wao wawe Wajumbe wa Baraza la Mapinduzi kwa nini tuwanyime fursa hii wakati Katiba imewapa nafasi kama ni wasaidizi. Jambo hili linakosesha utawala bora kwetu Zanzibar.

Leo Mhe. Spika, nilipokuwa nikisikiliza Bunge Mhe. Naibu Waziri aliwasilisha hotuba ya Mhe. Waziri ambapo hapa si rahisi, hapa ni lazima Waziri asimame pale. Lakini kutokana na nguvu alizopewa kwa mujibu wa Katiba Naibu Waziri anachukua nafasi zote ambazo waziri anaeleza.

Hapa panahitaji marekebisho makubwa. Wizara yako inahitaji kuishauri serikali katika eneo hili. Ni lazima Manaibu Mawaziri kwa mujibu wa Katiba watumike kwa sababu wanaonekana wapo wapo tu na inafika pahala wanadharauliwa na hata Makatibu Wakuu. Makatibu Wakuu wanawaona si chochote si lolote, Manaibu Mawaziri wao kazi yao ni kujibu maswali tu. Hii haipendezi ni lazima tuwape nafasi kwa mujibu wa Katiba wafanye kazi zao za Wizara na wawe na heshima kamili. Hilo jengine Mhe. Waziri ni eneo moja kubwa la Kikatiba ambalo kwa hapa kwetu halifanyi kazi vizuri.

Eneo jengine nilikuwa nahisi linahitaji marekebisho kidogo ya Kikatiba. Ukiangalia Katiba yetu ya mwaka 1984 ibara ya 49 kifungu kidogo cha (1) Katibu wa Baraza la Mapinduzi. Ibara hii naomba ninukuu kidogo inasema kwamba:

Ibara ya 49 (i) “Kutakuwa na Katibu wa Baraza la Mapinduzi atakayeteuliwa na Rais na ambaye ndiye atakayekuwa dhamana wa Afisi ya Baraza hilo na dhamana kwa mujibu wa maelekezo atakayopewa na Rais kwa kupanga shughuli za mikutano pamoja na kuweka kumbukumbu na mikutano hiyo na kupeleka maamuzi yanayohusiana na watu au vyombo vinavyohusiana na atafanya kazi nyengine atakazopewa na Rais mara kwa mara. Katibu wa Baraza la Mapinduzi atakuwa ndiye Kiongozi wa watumishi katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar”

Mhe. Spika, kuna kasoro kwa nini Katibu huyu tunamwita Katibu Mkuu wa Baraza la Mapinduzi wakati Katiba haijaelekeza hivyo. Katiba inasema kutakuwa na Katibu wa Baraza la Mapinduzi leo tunampa cheo ambacho sio chake kwa mujibu wa Katiba. Huyu ni Katibu lakini ibara ya 50 inasema kutakuwa na Katibu Mkuu pale Afisi ya Waziri Kiongozi na Waziri yeyote anapokuwa na dhamana ya Wizara yoyote ya serikali, atakuwa ndiye msimamizi wa dhamana mkuu wa shughuli bila kuathiri mambo mengine.

Katiba imezungumzia Makatibu Wakuu wa Mawizara, leo tunamfanya Katibu Mkuu wa Baraza la Mapinduzi ndiye Mkuu wa Makatibu Wakuu tunakwenda sivyo au Katiba tuirekebishe. Kama tunamtaka Katibu Mkuu wa Baraza la Mapinduzi basi Katiba irekebishwe ili ionekane kweli ndio Katibu Mkuu kuliko wale makatibu wengine. Kitendo cha kumpa cheo ambacho si chake kwa mujibu wa Katiba ni kosa kwa mujibu wa Katiba. Hapa kama kuna marekebisho ya Katiba parekebishwe hapa ili huyu sasa kama tunamtaka ndiye awe Mkuu wa Makatibu Wakuu basi awe Katibu Mkuu kweli sio vyeo vya kupachika pachika.

Mhe. Spika, kuhusu suala la utendaji katika serikali. Mhe. Waziri amekwenda katika eneo hili na hili ni eneo linahusu utawala bora. Mimi nimpongeze sana kwamba eneo hili kaliona, ni eneo sahihi na kafanya utafiti kwamba kweli shughuli za utendaji katika serikali yetu ni dhaifu. Hili halina ubishi sote ni mashahidi kwa hivyo panahitaji usimamizi wa kutosha.

Mhe. Spika, leo unakwenda afisini saa 2:00, saa 3:00 watu hawajafika kazini, halafu tunahubiri maendeleo, maendeleo yatakujaje wakati hakuna uwajibikaji katika maeneo ya kazi, unakwenda ofisini saa 7:00 hakuna mtu au unakuta afisi ina watu 6, 7 unamkuta mmoja kabakia pale. Hivi tuseme ndio hakuna kazi za kufanya? Kwa hivyo eneo hili umeliona ni eneo muhimu sana katika visiwa vyetu vya Zanzibar, bado hakuna uwajibikaji mzuri katika vyombo vya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Spika, linalosikitisha hata katika maeneo ya mapato unakuta mrundikano wa watu katika maeneo ya mapato wanamsubiri karani yule wa kukusanya mapato unaambiwa karani hajafika, karani hayupo saa 4:00, saa 5:00 watu wamerundikana pale, basi hata kupokea pesa nazo tunaona taabu.

Mimi naamini Wizara yake ya Utawala Bora kama nilivyozungumza mwanzo ni Wizara mtambuka inaweza ikachukua nafasi hii kuhakikisha kunakuwa na uwajibikaji katika serikali. Ndio maana tumesema Wizara ya Utawala Bora ni Wizara Mtambuka ina haki ya kwenda katika maeneo yote ili kuona kwamba utawala bora unakuwepo. Hatuwezi kuzungumzia suala la utawala bora wakati wafanyakazi hawafanyi kazi.

Pamoja na ufanyaji wa kazi Wizara hii pia nayo inahusika kuona kwamba wafanyakazi wanapata maslahi yanayostahiki. Pengine kipato chao kidogo ndio kinachowasababisha washindwe kukaa ofisini. Lakini waziri hakulizungumzia kwenye *speech* yake kwamba mishahara ya wafanyakazi wa serikali ni midogo haikidhi mahitaji, matumizi yamekuwa makubwa kuliko kipato chao.

Mhe. Spika, Mzee wetu Ali Hassan Mwinyi wakati fulani alikuwa anazungumza kwamba "*Haki na Wajibu ni Watoto Pacha*" kwa hivyo wafanyakazi ili wafanye kazi vizuri ni lazima maslahi yao tuyaangalie. Wizara yako ihakikishe inaishauri serikali juu ya jambo hili kwa sababu pengine wanakuwa wanautumia muda ule wa kazi za serikali kwenda kujitafutia mapato mengine.

Mhe. Spika, mwisho nizungumzie suala la kaka yangu pale Mhe. Hamad Masoud alipozungumzia juu ya suala la *ballot* ile ambayo itakwenda kwenye kura ya maoni. Kusema suala la kuwekwa muundo wa serikali liondolewe, mimi sikubaliani na hoja ile.

Kwa nini sikubaliani nalo. Unapokwenda kumuuliza mwananchi juu ya kwenda kwenye serikali shirikishi ni lazima aelewe muundo wa serikali yenyewe. Sisi hatukuzungumzia tu suala la serikali shirikishi kwamba tuwe na serikali shirikishi lakini pia tumezungumzia na muundo wenyewe uwe vipi.

Kwa hivyo ni wajibu wa Tume ya Uchaguzi kuhakikisha wananchi wanaelewa huo muundo wa hiyo serikali shirikishi utakuwa na muundo gani, Serikali ya Umoja wa Kitaifa inakuwa vipi. Kwa hivyo ni tume ya uchaguzi ni wajibu wake kwenye *ballot* na hata ukiangalia kwenye sheria inaelekeza kuwa Tume ya Uchaguzi ihakikishe kwamba wananchi wanaelewa. Unapomwambia mwananchi tu kwamba tutakuwa na mfumo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Atakuuliza itakuwaje? Kwa hivyo ni wajibu kuelekezwa kwamba kutakuwa na mabadiliko ya muundo kwa sababu itakapokuja Serikali ya Kitaifa nayo ina muundo wake. Ni wajibu wa Tume ya Uchaguzi kuwafahamisha watu na *ballot* iwemo kwamba waelewe huo muundo wa Serikali ya Kitaifa.

Mhe. Spika, kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Magomeni tunaunga mkono kwa asilimia mia hotuba hii na tunamtakia kheri Mhe. Waziri katika shughuli zake za kila siku. Ahsante.

**Mhe. Ali Moh'd Bakar:** Mhe. Spika, awali ya yote nichukue nafasi hii pia nimshukuru Mwenyezi Mungu (SW) kwa kutuwezesha kufika hapa saa hizi tukiwa hai na Mwenyezi Mungu akaturuzuku na uzima ambao umepelekea kufika hapa ambapo hivi sasa hivi tupo.

Mhe. Spika, pia nikushukuru na wewe katika hali ya kukupongeza kwa kunipatia nafasi hii ili na mimi nitoe mawazo yangu kwa uchache sana kama utaratibu ambao tumejipangia. Pia nampongeza Waziri kwa kuwasilisha hotuba yake hii ya Wizara ya Nchi (AR), Katiba na Utawala Bora.

Nataka nichangie hotuba hii kwa ujumla sana hii dhana ya utawala bora kulingana na vile ambavyo mimi naona au nafikiria. Dhana ya utawala bora mimi naiona inajengeka katika misingi mikuu labda mitatu:-

1) Mahakama
2) Haki za kiraia na
3) Masuala ya Tume za Uchaguzi

Mhe. Spika, katika nchi yoyote duniani ili ionekane kwamba inafikia katika masuala ya utawala bora ni lazima haki za raia wake ziheshimiwe na ni lazima raia wa nchi ile wajivunie utawala wao na wajivunie maslahi ya nchi yao. Tukifanya hivyo basi tunaweza kupiga hatua moja tukaona kwamba haki za raia ni zipi na wale ambao si raia lakini wanaishi katika nchi ile ni zipi.

Mhe. Spika, leo ukenda hapo Kenya tu basi unaona ni kiasi gani raia anaweza kupata haki zake ndani ya nchi ile. Lakini sisi hapa kwetu bado hatujafika hapo. Hapa hata ukiangalia kwenye taasisi za serikali nyingi utawakuta wageni wamepewa *priority* kuliko hata wenyeji. Hili ni jambo ambalo halipelekei kuona kwamba sasa hivi tuna utawala bora.

Mhe. Spika, zinaweza kuwa ni chachu ya kuharibu dhamira nzuri ya serikali juu ya dhana hiyo ya utawala bora. Mahakama inapozibinya haki kutokana wale wanaoshtakiwa basi unaweza kuona ni kiasi gani dhana hii ya utawala bora haipatikani. Lakini pale mahakama inaposimamia haki unaweza kuona ni kiasi gani inaweza kusimamia haki ya utawala bora na kwamba kila mtu anapata haki yake kwa mujibu wa lile analostahili.

Mhe. Spika, leo ukenda kwenye mahakama zetu basi ama ujulikane au uwezo kwa kiasi fulani lakini kama huna uwezo basi hiyo inaweza kukupelekea usipate haki yao na wakati mwengine ukatafutiwa kosa ili uadhibiwe.

Mhe. Spika, ukiacha hilo mara nyingi huwa nasikia kuna wezi wa kuku au ndizi hufungwa miezi sita au mwaka au miaka mitatu lakini watu ambao wanafanya matokeo makubwa makubwa hapa na wanajulikana wanaachwa kwa sababu ya uwezo wao au kwa sababu ya watu ambao wapo mbele wanawasimamia. Hapa panaweza kudhoofisha jitihada za Wizara au za Serikali kufikia huko, watu wachache wanaweza wakatia doa kubwa na kupelekea kutokufikia malengo haya ya utawala bora.

Mhe. Spika, Wizara hii imegusa katika kila eneo maana yake ni bahari. Wizara iliyopita juzi ni Wizara ya Vikosi, kuna mambo yaligusiwa na ambayo Wizara hii pia inawagusa kwa sababu inayotoa haki kwa mujibu wa tokeo lilivyo ni Mahakama.

Pale Kiinuamiguu palitajwa kwamba kuna watu wamo mle ndani ama wamefungwa na kuna watoto wengine wamo mle ndani ambao wana umri mdogo wamechanganyishwa na watu wakubwa ambao wanawafanyia vitendo viovu. Tunapotaka kwenda katika utawala bora humu mote ni mwahali mwa kumuangalia je, watu wanatendewa haki.

Mhe. Spika, mimi nikupe mfano mmoja. Hivi wewe kama una kuku wako majogoo wa kienyeji unawafuga halafu ukenda kutafuta kuku wake (makoo) wanne au watano halafu ukawaambia watu mimi nimechukua kuku wangu wanne au watano makoo nakwenda kuwapiganisha na hawa majogoo. Hivyo unakusudia ukawapiganishe au wakapandwe wazae na kuwachukua watoto wadogo ukenda ukawatia pamoja na majambazi ukawaweka pamoja mle, mnakusudia wale watoto waharibiwe ndio maana yake.

Ndio maana hicho ndio kilichokwenda kuonekana wakati Kamati yako ilipokwenda kufanya ukaguzi pale jela waliwakuta watoto wengi wameshaharibiwa Mhe. Spika. Kwa sababu wamewekwa pamoja na majitu makubwa na ambayo hayajali chochote yanawaharibu wale watoto.

Taifa lile, wale wamepelekwa pale ama kwa makosa yao madogo madogo au kwa sababu mbali mbali za mitaani. Kwa hiyo wanafanya vitendo visivyo halali unategemea nini? Unategemea baadaye watakapotoka mule watakuwa wamejifundisha nini? Kwa hiyo ile dhana ya utawala bora hapa Mhe. Spika, itakuwa imekwenda kombo.

Mimi nadhani Mhe. Waziri ana jukumu kubwa na ana jukumu kubwa la kuangalia katika kila *department* ya Wizara hii kwa sababu imegusa kila eneo ahakikishe anaingia bila ya kujali kwamba mtu fulani kapewa dhamana gani, madamu imetajwa utawala bora ahakikishe kwamba haki inatendeka kila pahali, haki mtu anatendewa kila eneo.

Jengine Mhe. Spika, hapa kuna hivi vitambulisho vya Mzanzibari. Kuna wengine wana haki za kimsingi Mhe. Spika, ambazo zile ndio haki za kinchi zitakazompelekea Mzanzibari kupata haki zake za misingi lakini kuna wengine hawajapewa. Kwa hivyo ile dhana ya utawala bora hapa inapotoshwa hawajapewa kwa sababu mbali mbali.

Mimi naamini Waziri yeye hana ubaya na mtu yeyote lakini ni wajibu wake kusimamia na ni wajibu wake kuliona hili kwamba zinapokuja haki za kinchi kila mmoja apate haki yake kwa mujibu wa taratibu zilizopangwa.

Si vizuri kupanga sheria, kupitisha sheria halafu wakati wa utekelezaji sheria zile Mhe. Spika, wakaja wakazipata haki zile watu wachache au wengi lakini wengine wakaachwa kwa sababu ama za kisiasa au vyovyote vile. Mimi nadhani hapa itakuwa hatuwatendei haki kwa sababu katika suala la kinchi, nchi zote duniani unazotembea unazokwenda basi utakuta kwamba raia amepewa *priority* zaidi kuliko mgeni.

Mhe. Spika, zamani Oman wakati wale Waraabu hawajasoma ilikuwa ukenda kule kwao watu wengi kutoka huku Afrika ndio wanaofanya kazi, lakini baadaye walipokuja kusomesha watu wao kule, Waafrika wote waliwatoa yule ambaye ana sababu maalum ya kufanya kazi lakini wengi zaidi hata ukenda mtu huwezi kupata kazi kule kwa sababu wanapewa *priority* wazawa. Sisi hapa kwetu sio hivyo ni lazima na sisi tubadilike ndio tuseme kwamba sasa tunakwenda katika misingi ya utawala bora.

Mhe. Spika, kuna baadhi ya maeneo tumeweza na tutaendelea, nadhani kwa sababu hii dhana bado ni mpya tutafika mahali tutaweza ikiwa tutaongoza kwa nia njema. Mfano hapa kuna Afisi ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali. Mhe. Spika, hapa tumeweka hii Afisi inafanya kazi zake kwa uadilifu, uwazi na pale ambapo anapolazimika kuishauri serikali kuikemea anaikemea bila ya kujali kama yeye ni mwanamke au bila ya kujali lolote, anafanya kazi zake kwa uwazi sana.

Hapa kwa kweli panaweza pakaleta chachu ya maendeleo lakini panaweza pakaleta mwelekeo wa kuonesha kwamba tunatoka wapi, tupo wapi na tunakwenda wapi. Huyu mama na vijana wake, akina Shekhe Muhyddin na vijana wengine wanafanya kazi kwa uwazi sana bila ya kujali aliyemueka ni nani, ana cheo, zaidi yeye anafanya kazi kwa mujibu wa taratibu na sheria zilizopo zinazomuongoza hafanyi kazi kwa sababu ya shindikizo la mtu. Hapa kwa kweli tumeweza na ni pahali pazuri.

Mhe. Spika, naamini kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu tunaweza tukafikia huko tunakokuhitaji kufikia ikiwa nia zitakuwa ndizo. Mimi nimuombe Mhe. Waziri kule Wilaya ya Micheweni katika Mahakama ya Kadhi, pale atuletee Kadhi kwa sababu kuna kesi nyengine hazihitaji sheria hizi tulizozipanga humu, zinahitaji sheria za kidini.

Kuna watu wengine huko wamegombana mke na mume wanahitaji wende kwa Kadhi lakini haipatikani sheria ile bali panapatikana dhulma kwa sababu ama

mke analalamika au mume. Unakuta kwamba hakuna haki inayopatikana kwa sababu hakuna wa kuhukumu au hakuna wa kufikiria zile kesi. Kwa hivyo mimi hapa hakuna wa kuhukumu au hakuna wa kufikiria zile kesi. Kwa hivyo hapa nimuombe Mhe. Waziri pamoja na mambo mengi ambayo tumemkabidhi afanye mpango apate kazi kule ili aende akasimamie hizi kesi, kwa sababu kuna mambo mengi ambayo yanajitokeza.

Mhe. Spika, Afisi ya Mufti nayo ina kazi nyingi, ina hukumu na ina changamoto kubwa ya kusimamia masuala yote ya kidini nchini, kama alivyosema hapa Mhe. Hamad Masoud kwamba eti kuna haki za watoto na kutakuwa na Mswada utaletwa hapa. Sijui ifike wakati kwamba nimeshamwambia mwanangu, halafu mtoto wangu kamkosea Mhe. Mansour, eti nikimpiga atakwenda kusema kwamba baba yangu amenipiga, niende nikafungwe.

Mhe. Spika, mimi nataka nije kufungwa hasa kwa kumpiga mtoto wangu. Mimi ikiwa mtoto wangu niliyemzaa kama atakuja kunikosea halafu nipite wewe usinambiE, lakini nijue tu kwamba huyu mtoto ameshamkosea Mhe. Spika, basi mimi nitampiga hapo hapo.

Kwa hivyo, akenda kunishtaki niko tayari nifungwe Lakini jambo hili litatupeleka pabaya sana kwa sababu hakuna kitu kibaya kama kutokujali umaskini na unyonge wako, ikishakuwa unyonge wako huuamini aliokupa Mwenyezi Mungu ikawa kila kitu unaridhia tu, hivyo sivyo.

Mhe. Spika, Mwenyezi Mungu kaumba njia mbili tu na kila kitu pia amevifanya viwili viwili, Uislamu ameuweka na Ukafiri, Mke amemuweka na Mume, jua ameweka na mvua, usiku ameuweka na mchana na utajiri ameuweka na umaskini, kila kitu viko viwili viwili. Mhe. Spika, hiki ni kisiwa tena chenye asilimia kubwa sana ya Waislamu, kwa hivyo tutakapoingiliwa kwa sababu juu ya unyonge wetu kwani sisi ni wanyonge lakini hatujaadhirika kwa mtu.

Mhe. Spika, hatuadhiriki kwa sababu ya kuamini unyonge wetu. Hii ndio dhana ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na hapo zamani kabla ya mapinduzi ilikuwa watu wanadhalilishwa tu, ilikuwa unaweza kupangiwa kitu chochote kile ukifanye. Lakini baada ya mapinduzi ya Januari, 1964 kwa kweli mambo mengi yaliondoka na yakatoa uhuru kwa Wazanzibari kufanya mambo yao yote.

Mhe. Spika, leo tunatoka kule kwenye dhana ile matokeo yake kwamba tunawasaliti wakuu wa mapinduzi. Mhe. Spika, leo tunakwenda kuridhia mikataba ya kikafiri kwa sababu ya unyonge wetu halafu inakuja kupangiwa

sheria mpaka watoto wetu eti ukimpiga mtoto akenda kukushtaki unachukuliwa hatua. Kwa hivyo, Mhe. Spika, tukiyachukua haya sisi hapa petu yatatupeleka pabaya kwa sababu sisi hapa ni wanyonge.

Mhe. Spika, mambo mengine hayafai kuigwa hapa petu. Tukishakuiga mambo ambayo sio, nina hakika tutakaa pahali pabaya. Kwa hivyo, ile dhana ya utawala bora kulingana na silka, mazingira na imani yetu tunayoifuata basi hapa itakuwa sipo.

Afisi ya Mufti hapa ina kazi kubwa ya kuielimisha jamii juu ya kutoa mawazo yake kwa mujibu wa dini yetu kwa serikali na kuieleza kwamba kuna baadhi ya mambo tuyafuate na kuna baadhi ya mambo hayafai kufuatwa, kwa sababu mambo haya yakishakuingia katika jamii kuondoka kwake itakuwa ni vigumu mno. Mhe. Spika, sasa itakuja kuwa kwamba baba hana haki tena ya kumpiga mtoto wake endapo amekosa.

Mhe. Spika, jambo hili lazima tukae tufikirie la kulifanya kwa sababu sisi kuna siku tutaondoka katika dunia hii na tutakwenda kuulizwa na Mwenyezi Mungu ni namna gani vile tulivyokuwa tukivuchunga tumevichunga vyenginevyo tutakuwa hatuna jibu na Mwenyezi Mungu hakuadhibu mpaka akumalize utakapokuwa huna hoja. Mhe. Spika, mwisho kabisa ni kwamba Afisi hii ya Mrajisi Mkuu wa Serikali ni kwamba anadhalilika. Mimi ningelikuwa nina uwezo nisingemdhalilisha Mrajis Mkuu wa Serikali ningelimnunulia japo baiskeli akapanda.

Mhe. Spika, Mrajis Mkuu wa Serikali mimi nimeshamkuta mara nyingi anatembea kwa miguu, siku hiyo nimemkuta kwa Mchina nikamuuliza unakwenda wapi akaniambia nakwenda afisini sasa hivi. Mhe. Spika, kwa bahati mimi nilikuwa nina gari nikamchukua mpaka kwenye afisi yake.

Mhe. Spika, mimi akiniruhusu Mhe. Waziri kama sio kosa au sikumdhalilisha basi ningemtafutia baiskeli, hili sio jambo zuri imekuwa bora Sheha ndiye mwenye thamani kule Mrajis Mkuu wa Serikali. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri aone kwamba ipo haja kuhakikisha kwamba Mrajis Mkuu amepatiwa usafiri kwa ajili ya kufanya kazi za serikali kwani ana kazi kubwa, ana majukumu mazito hivyo katika dhana ya utawala bora ni pamoja na kusimamia majukumu ya watendaji wetu ili kuwapa nafasi na uwezo wa kufanya kazi zao.

Mhe. Spika, ukiangalia hali ya kawaida ni kwamba watendaji wetu wote wanafanyakazi kwa kujitolea zaidi, ikiwa watakuwa na imani hiyo basi kuna mambo madogo madogo tuwasaidieni kama vile usafiri ili zile kazi wazifanye vizuri zaidi.

Mhe. Spika, kwa sababu kiwango cha mshahara kinachotoka, maslahi ya mshahara ni madogo zaidi kuliko kazi wanazozifanya. Kwa hivyo, kuna mambo madogo madogo tuwasaidie ili wapate nguvu ya kuzifanya kazi zao kwa ajili ya kuikomboa nchi yetu na kwa ajili ya kufikia ufanisi.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo namuomba Mhe. Waziri akija hapa aniambie kwamba Mrajis Mkuu wa Serikali kama atampa gari au kama hampi aniambie mimi nimtafutie japo baiskeli. Ahsante sana Mhe. Spika naunga mkono hoja.

**Mhe. Ali Abdalla Ali:** Ahsante Mhe. Spika, na mimi nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kutoa mchango wangu katika hotuba hii ya Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora. Kwanza nimshukuru Mhe. Waziri na kumpongeza kwa kuweza kuleta hotuba fupi sana lakini amekusanya mambo yote ambayo yamo katika wizara yake na pia niwapongeze watendaji wake ambao walimsaidia kutekeleza na kuandika bajeti hii ya mwaka 2010/2011.

Mhe. Spika, mimi mchango wangu katika hotuba hii nitaanza ukurasa wa 14 kifungu cha 29 kuhusu Mahakama. Mhe. Spika, kidogo nimefanya hofu na nilikuwa nataka nimshauri Mhe. Waziri pamoja na Mashekhe waliokuwepo watusaidie hii kazi hapa naomba ninukuu kidogo halafu nitoe wasi wasi wangu.

> "Mhe. Spika, katika kipindi cha Julai, 2009 hadi Machi, 2010 jumla ya kesi 5,472 zimefunguliwa katika Mahakama mbali mbali Unguja na Pemba, ambapo kesi 1,229 ni za madai na 4,055 ni za jinai. Kiasi hiki ni ongezeko la asilimia 22.6 ukilinganisha na mwaka uliopita".

Mhe. Spika, kwa maelezo haya inaonesha bado uhalifu unakua hapa petu badala ya kupungua. Sisi tumeona tumeweka watu mbali mbali wa kuweza kuisaidia serikali kutoa taaluma kwa wananchi wetu ili maasi mengi yapungue, lakini kila bajeti ikija inaonesha maasi yanaongezeka. Mhe. Spika, kwa sababu kila kesi zikifunguliwa nyingi basi pengine wizi na maaasi mengine yanaongezeka.

Ningemshauri Mhe. Waziri tutumie Mashekhe wetu na sisi viongozi kwenye jamii ili tuweze kuelimisha wananchi wetu kwamba twende katika mambo ya kheri, tupendane, tuache kufanya mambo ya maasi ambayo mtu yanaweza kumpeleka pahala pabaya. Nadhani tukijitahidi sote tunaweza tukapunguza wimbi hili la kuongezeka kwa kesi.

Mhe. Spika, kama kazi hiyo haikuweza kufanyika pande zote mbili basi nadhani watakaojaaliwa kufika mwakani hizi kesi zitazidi. Mwisho itakuwa kama aibu kwenye nchi yetu labda hatwendi katika utawala bora. Mhe. Spika,

namuomba Mhe. Waziri kwa jitihada zake zote ajitahidi atumie vyombo vinavyohusika kuelimisha jamii juu ya kukwepa haya maasi ambayo yanasababisha mtu kushtakiwa na kufunguliwa kesi.

Mhe. Spika, nikiendelea katika ukurasa mwengine katika kifungu cha 30 kufanya matengenezo ya majengo ya Mahakama. Mhe. Spika, nashukuru kwamba majengo yetu mengi ameyataja humu yamefanyiwa matengenezo na sasa hivi yameweza kutumika kwa uzuri. Umetaja jengo la Vuga, Mwera na sasa hivi Tunguu pia kuna ujenzi wa Mahakama.

Mhe. Spika, na mimi pale petu Mfenesini tunayo Mahakama kipindi kirefu tangu ukoloni na kila tukija kwenye bajeti hutiwa kwamba imo kwenye matengenezo, na imegaiwa ukuta upande wa pili lakini naona haijesha. Mimi niliwahi kushauri mwaka jana kwamba pale sasa hivi pameshakuwa finyu ajali nyingi zinatokezea na kesi huwa nyingi watu wanajaa mpaka barabarani.

Mhe. Spika, nikasema kwa kuwa nina eneo lile ni Mwakilishi nina uwezo wa kutoa kiwanja ili pale tuhame tutafute pahala pazuri pajengwe pawe nafasi ya kutosha, na kila mtu atafanya kazi yake kwa utulivu kuliko hivi sasa karani humo, jaji humo humo na hakimu humo humo ilimradi mashaka matupu. Mhe. Spika, niliwahi kupewa mtu siku moja tukakague lakini mpaka leo naona kimya. Kwa hivyo, sijui mheshimiwa mmeogopa kwa kuwa hamna fedha za kujengea au mawasiliano yalikuwa mabaya.

Kwa hivyo, na leo naomba tena kwa vile nimepata nafasi katika wizara yako kuchangia bado mimi adhma ya kusaidia ninayo. Namwambia Mhe. Waziri atakapopata nafasi anipe japo Afisa wake tutakwenda kuangalia na wahusika watapima halafu tujenge jengo ambalo liwe la kileo. Mhe. Spika, hili nakuomba ulifanyie kazi na utakapokuja kufanya majumuisho kidogo unitie tamaa umekubali ama umekataa.

Mhe. Spika, nikiendelea katika sehemu hiyo ya Mahakama kabla sijenda sehemu nyengine kipindi kile pia tulichangia suala hili kwamba Mahakimu wetu bado vipando hawana na inawezekana mimi nimeshtakiwa lakini *lift* ninayo namchukua mjini mpaka shamba. Mhe. Spika, utakuta kufadhiliwa nako uso unaumbwa na haya.

Mhe. Spika, tulishauri kwamba wenzetu hawa wanaofanya kazi nje ya mji basi watafutiwe vipando ende kwa uhakika afike pale hapana upendeleo akitoa uamuzi wake kufuatana na vitabu vyake vya sheria inajulikana kwamba yule amefanya kazi kadiri inavyotakiwa. Lakini leo kwa utaratibu huu tunaokwenda nao sio mzuri hata kidogo. Mhe. Spika, tunashauri na hili litizamwe pande zote mbili kumsumbua mfanyakazi na pia kumuweka katika hali ya usalma wa kazi

yake. Tunaomba hili lizingatiwe wenzetu hawa wapatiwe vipando ili waweze kufanya kazi zao kwa uhakika.

Mhe. Spika, nikiendelea kwenye hotuba hii nije kwenye ukurasa mwengine wa 37 Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali. Hapa ameeleza kwamba Mrajis anahusika na shughuli mbali mbali, moja ni uandikishaji wa vizazi na vifo, jengine ni kuandika ndoa na talaka na mambo mengine. Nimeyataja haya mawili nataka niyazungumze.

Mhe. Spika, nashukuru kwamba suala la usajili wa vizazi na vifo ni jambo zuri kwa kila nchi kwa sababu mtu anajua kwanza ni watu wangapi wanazaliwa na wangapi wanakufa. Katika masuala ya maendeleo mnaweza mkajipangia mkawa mnakwenda vizuri. Mhe. Spika, nimebaini tatizo kubwa hivi sasa ni kwamba kama mtoto amezaliwa hospitali kuna kitambulisho fulani anapewa, halafu ukifika muda fulani anakwenda kuchukua karatasi yake ya kuzaliwa.

Hapo unajua maisha ya wenzetu ya vijijini mtu anaweza akachukua akaiweka pahala, mtoto amefika umri wa kwenda skuli anaitafuta haioni, hilo sio jambo zuri ukirudi kunakohusika ukenda kuitaka tena utaambiwa kwanza utoe faini, na faini iliyokuwa pale sitaki kuitaja lakini kwa watu wanyonge ni kubwa kidogo. Mhe. Spika, hapo pana matatizo mawili lakini yote yanachanganywa kwa hukumu moja.

Mhe. Spika, mimi nimechukua lakini baadae imepotea pengine kwa kuhama hama ama pengine nyumba ilibomoka unajua nyumba za kishamba tena, lakini kuna mwengine anaweza kufika umri kama wangu mimi lakini bado hajawa nayo. Pengine mtu kapata nafasi ya kazi pahala akaambiwa lazima ulete cheti chako cha kuzaliwa hapa ndio upate kazi.

Hapa mimi nadhani itakuwa ni kesi mbili tofauti, wangekaa wahusika wakatathmini tena mtu ambaye aliwahi kuchukua na ikapotea kwa bahati mbaya na mtu ambaye hakuchukua na alikuwa anajua kile kitu ni muhimu ukawachanganyia adhabu.

Hili itakuwa sio jambo zuri wangekaa wataalamu huyu aliyekuwa amejisahau anapokumbukia awe ana adhabu kubwa na huyu ambaye alichukua kimempotea anarejea tena na kumbukumbu zipo naye kidogo izimuliwe hiyo adhabu isilingane. Hilo litatusaidia sana.

Mhe. Spika, jengine la upande wa vifo si watu wengi mtu akafiliwa akenda akatoa taarifa kama amefiliwa kwa Sheha au kwengine. Naomba na hili lina faida kubwa kwa nchi lazima bado taaluma itolewe ili watu wafahamu kwamba mtu pia akifa akitolewa taarifa anajua kuweka kumbukumbu vizuri katika

mipango ya maendeleo ya nchi yetu. Hili bado panataka mkazo na taaluma ili watu waelewe faida yake.

Mhe. Spika, nikija kwenye upande wa ndoa na talaka hapa kidogo sasa hivi kumezuka matatizo na wenzangu wamezungumzia sheria. Mimi juzi yamenikuta hayo nilikuwa na Mhe. Mohamed Ali Salim. Mhe. Spika, tuna Msikiti wetu hapa tunaita Msikiti-udi huwa tunakwenda kusali siku ya Ijumaa ukiingia mle ukitoka na wewe unanukia udi hiyo sio mbaya lakini juzi kulitolewa mawaidha mpaka tukawa tunatizamana, laiti kungekuwa na Msikiti karibu mimi ningetoka.

Mhe. Spika, walikuwa wanasema hasa wamo humu humu na wataipitisha keshokutwa lakini tutakutana mbele ya Mwenyezi Mungu huko. Mhe. Spika, sisi wawakilishi tulikuwa tunatizamana tena sote tulikaa mstari mmoja, hotuba ilikuwa kali mpaka ndani ya mwili unasisimka. Nikaona jamani sitakuja kupigwa lakini kwa bahati nzuri ujumbe umefika. Mhe. Spika, mimi nilikuwa nashauri wenzetu Mashekhe kama likitokea tatizo serikali ipo tusingojee Misikitini inakuwa mnatutoa imani.

Mhe. Spika, nasema hili suala kweli lipo lakini sheria haijaja hapa petu basi kama lina tatizo muda bado upo washauriwe wanaohusika warudi wakakae ili likija hapa petu pasiwe na mambo kama hayo tukafikishana mpaka mbele ya Mwenyezi Mungu.

Naomba mambo haya yarekebishwe kidogo, Mashekhe wakipata kitu kama kimekwenda vibaya pasitolewe lawama wakati kitu hakijaja. Kwa hivyo, naomba hilo sio jambo la mzaha kwa sababu linatokota sasa hivi liko jikoni, kwa hiyo tukilipika vibaya litaungua litakuwa haliliki, lakini tukilipika vizuri litalika.

Mhe. Spika, jambo jengine hapa ni kwamba kumetokea matatizo sasa hivi hiyo sheria haijaja, lakini kwenye Afisi ya Kadhi sasa hivi yanakwenda mashtaka. Mhe. Spika, sasa hivi vijana wamepata uhuru mtu anaweza akatafuta pengine mpenzi wake wakakaa wakasoma wakamaliza lakini kutokana na nyendo anazokwenda akenda kupeleka posa nyumbani anakataliwa.

Kwa hivyo, mtoto kama huyo akikataliwa na wazazi wake huwa anakwenda Afisi ya Kadhi anasema kwamba nimeleta mume wangu amekataliwa kwa hivyo naomba nitazamie kama kidini inawezekana niozeshe. Mhe. Spika, na Kadhi naye anajitwika mzigo anamuozesha wakati kumuozesha mtoto lazima mwenye idhini atoe kwamba namuozesha mtoto wangu kwa fulani bin fulani na kwa mahari waliokubaliana.

Sasa hivi kesi zimekuwa nyingi, Makadhi wanachukua kesi kama hizo halafu watoto wanaachiwa radhi siku tatu wanakuwa wendawazimu, maradhi yanakuwa mengi kumbe baba hakuridhika na mtoto wake. Mhe. Spika, inakuwa hizi afisi zetu badala ya kutengeneza wao wanatenganisha baina ya familia na familia.

Namuomba Mhe. Waziri hili tatizo lipo nakuomba ulifuatilie ili mlirekebishe kwani jamii sasa hivi inateketea kwa sababu kama mtoto atakuwa na haki anakwenda kwa Kadhi wakati huku nyumbani amekataliwa mume na kule anaozeshwa hapo inakuwa umeshamtenganisha na familia yake.

Mhe. Spika, sasa hivi mtoto kama huyo anakuwa anajiona mzima lakini endapo mfano akiumwa inakuwa ni matatizo, kwani wazee ndio wakumshughulikia na wazee wake wameshamtenga, hivyo atashughulikiwa na nani. Naomba jambo hili lishughulikiwe kwenye jamii zetu lipo kwa hivyo tulifanyie kazi ili matatizo hayo yanayotokezea tuyawahi kabla hayajakuwa makubwa.

Mhe. Spika, nikitoka hapo nije kwenye ukurasa mwengine wa 48 kuhusu Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana. Mhe. Spika, hapa nilikuwa nataka nizungumzie kwamba Kamisheni hii inahusika na mambo mengi yametajwa kisheria ya kusimamia mali za wakfu, amana, mirathi ya Waislamu, sala, Mabaraza ya Iddi, Hijja, Zakka, misaada na kadhalika.

Mimi nataka kusema kwamba hivi sasa kuna watoto wengi ambao ni yatima katika nchi yetu na wenzetu wanashughulikia mambo mbali mbali wamezungumza hapa na ziko *NGO's* zinasaidia watoto yatima kwa kuwasomesha, kuwatafutia nguo na mambo mengine. Lakini utakuta afisi yetu hii haishughulikii sana mayatima katika misaada inategemea *NGO's* zilizoanzishwa.

Kwa hivyo, ningelishauri kama uwezekano upo wangefungua na wao kitengo cha kuweza kusaidia yatima. Kama mtu amefiliwa anapeleka cheti cha kifo cha baba, inapelekwa targisi ya mtoto anajuulikana umri aliokuwa nao ili wakaweza kusaidiwa angalau akifika kwenye miaka 18 mtoto akajiendeleze mwenyewe. Sasa hivi ukenda kwenye hizo *NGO's* zinakuwa zina mizunguko mingi mpaka unapata ule msaada.

Nadhani na nyinyi mngeangalia kama uwezekano upo mgetafuta wafadhili mkaweka kitengo tukaweza kuwalea watoto yatima kuanzia umri wa miaka 2 mpaka 18, baadae wakishajiweza wakaweza kujiendeleza wenyewe. Nadhani itasaidia zaidi ama si hivyo basi hizi *NGO's* zingeongezwa wakashawishiwa watu wakazidi kufungua zisiwe moja au mbili. Mhe. Spika, naomba hili kama

litaweza kufanyiwa kazi nitakushukuru sana kwa sababu tutaweza kuwalea watoto wetu na wao watapata haki katika nchi yao.

Mhe. Spika, nikija kwenye ukurasa mwengine wa 49 nilikuwa nataka nizungumzie suala la mashamba ya wakfu. Hapa inaelezea kwamba kuna mashamba yanasimamiwa na yanachangisha fedha kidogo, hivi karibuni bodi ya sehemu ya afisi hii ilipita kukagua mashamba mbali mbali lakini humu imetaja mashamba manne tu na vikataa. Sasa sijui yaliyokaguliwa hivi juzi yalikuwa hayamo kwenye matatizo haya, kama yamo nataka nielezwe.

Mhe. Spika, jengine la mwisho humu imeelezwa kwamba hizi mali za wakfu zinakuwa zinakodishwa kwa taasisi mbali mbali. Hapa pana deni la shilingi milioni 13,900,000 ambazo zinadaiwa afisi mbali mbali katika nchi yetu hii, hasa taasisi za kiserikali. Kwa hivyo, naomba na hili Mhe. Waziri kwa kuwa hiki kitu kimewekwa kwa kukusudia jambo fulani halafu bado panakuwa pana deni kidogo inatia unyonge. Kwa hivyo, ningeliomba taasisi zinazodaiwa wangelipa hizi fedha ili yale malengo yakafikiwa yaliyokusudiwa kwa sababu mtu anaweka mali kama hii isaidie mayatima halafu wewe unamkopa, hiyo inakuwa sio nzuri.

Kwa hivyo, naomba hizo taasisi zote na watu binafsi ambao wanadaiwa basi wahakikishe kulipa hili deni ili malengo ya wakfu yapatikane kwa vizuri. Mhe. Spika, baada ya hayo machache mimi mwenyewe binafsi pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Mfenesini naiunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja.

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Spika, na mimi nakushukuru kunipa nafasi hii ya kutoa mchango wangu japo nitakuwa na machache mno. Kwanza nataka nimpongeze Mhe. Waziri kwa kutuandalia kitabu ambacho kina nakshi za peke yake, maana vitabu vyengine nimeviangalia lakini hiki cha Mhe. Waziri huyu kina nakshi nzuri ambayo inapendeza.

Mhe. Spika, mimi kwa ufupi nataka nizungumzie hii dhana ya utawala bora. Kimsingi kitabu kimefafanua dhana ya utawala bora na misingi yake, lakini nimekuwa nikipata taabu sana kuona kwamba itazungumzwa dhana hii zaidi ni kwa maneno sio kwa vitendo. Nataka nimpe mfano Mhe. Waziri midogo sana lakini ni dalili kwamba hatujakuwa na umakini wa kufanya suala zima la utawala bora. Niseme kwamba tuangalie hapa Barazani.

Mhe. Spika, tangu juzi hii barabara ya Baraza la Wawakilishi ilikuwa haifungwi, kwa nini? kwa sababu ndani hamna Waziri Kiongozi wala Naibu Waziri Kiongozi. Leo nilipokuja asubuhi nikawaambia wenzangu hapo nje kwa sababu njia leo imefungwa ndani itakuwa Waziri Kiongozi yuko au Naibu

Waziri Kiongozi, na kweli nilipoingia ndani nimewakutia viongozi wetu. Suala ni kwamba jee, njia ile hufungwa kwa sababu gani? kwa sababu Waziri Kiongozi na Naibu Waziri Kiongozi au kwa sababu ya shughuli za Baraza kama muhimili wa dola.

Mhe. Spika, ikiwa jambo hili dogo hatuwezi kuli-*control* ni dhahiri kwamba dhana ya utawala bora ni maneno zaidi kuliko vitendo. Mhe. Spika, nikitaka Mhe. Waziri aniambie ile barabara inafungwa kwa misingi gani, hilo naomba nijue.

Mhe. Spika, ambalo ningeligusia kwa dhana hii ni masuala ya itifaki. Nimekuwa nikishuhudia mikutano mingi ya serikali hupewa kipaumbele zaidi Naibu Waziri kuliko hata Spika au Jaji Mkuu. Hili jambo halipendezi hata kidogo naomba Mhe. Waziri ulifanyie kazi ili liende na utaratibu mzuri wa utawala bora na nidhamu ya serikali.

Mhe. Spika, jengine ambalo nimetishika sana, juzi kuna gazeti la Tanzania Daima lilimnukuu Mhe. Sophia Simba huyu ni Waziri wa Katiba anawaomba wanawake wa Tanzania ambao waume zao sio CCM basi wawanyime unyumba. Mhe. Spika, hili gazeti nimelichukua ili kumuonesha Mhe. Waziri kwamba Tanzania Utawala Bora ni nadharia zaidi kuliko vitendo. Mhe. Spika, Mhe. Sophia amesahau kama hata CUF wana wake zao CCM.

Mhe. Spika, inapoletwa dhana kama hii ndani ya jamii mtu aliyekuwa hana uchambuzi wa mambo maana yake unaanzisha migogoro ndani ya jamii, jambo ambalo ni hatari kubwa. Huyu ni Waziri wa Katiba na Utawala Bora Tanzania anawambia wanawake wa Tanzania kwamba chaguzi hizi kama mume si CCM basi amnyime "nonino" sijui maana yake nini kama ni huo unyumba. Mhe. Spika, hii ni hatari namuomba sana Mhe. Waziri kwa Zanzibar hili suala likemewe kwa sababu Wazanzibari ni wachache na wameoana CCM na CUF. Mhe. Waziri nakuomba sana hili ulizingatie na huku ulipige vita ili Zanzibar hili lisije kwa sababu sio jambo zuri ambalo la utawala bora.

Mhe. Spika, jengine ni kuhusu Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana hapa nataka nigusie msikiti wa Chachani Chake-Chake Pemba. Msikiti ule wa Ijumaa pale Chachani ni msikiti wa wakfu chini yake kuna nyumba ambayo Wizara ya Elimu wanaitumia imewekwa wakfu pamoja na huo msikiti.

Mhe. Spika, hivi karibuni Katibu Mkuu Wizara ya Elimu amemtaka Afisa Mdhamini Pemba kwamba ile nyumba airejeshe awape Msikiti wa Chachani kwa sababu ni sehemu ya Msikiti. Lakini hadi leo nyumba ile Wizara ya Elimu wanaitumia na Afisa Mdhamini bila shaka amekataa kurejesha nyumba kwenye wakfu wa msikiti. Namuomba Mhe. Waziri hilo alifuatilie ili dhana hii ya

wakfu ipatikane vizuri na twende kwenye utawala bora. Mhe. Spika, haiwezekani nyumba ya wakfu ya msikiti ikatumiwa na Wizara ya Elimu na muda mrefu na hadi leo Afisa Mdhamini anagoma kuirejesha kwa watu wa Msikiti.

Mhe. Spika, jengine niende kwenye Afisi ya *CAG*, hapa niwapongeze sana kwa utendaji wao wa kazi, kwa kweli tumeanza kumaliza matatizo yote ya hesabu za serikali kwenye vitabu kwa muda mrefu. Sasa wanaendelea na kazi mwaka hadi mwaka lakini jambo ambalo ningemtaka Mhe. Waziri alifanye hii afisi nataka iongezewe uwezo wa kifedha kwa sababu wanahitaji sasa kufanya *value for money auditing*. Mhe. Spika, nchi hii sasa lazima iungane na nchi nyengine duniani wao waende kwenye ukaguzi wa mahesabu ya thamani ya majengo na mambo mengine.

Mhe. Spika, kwa mfano kama afisi hii ingekuwa na uwezo huo basi nadhani hata ile aibu ya juzi kule Pemba ya kuanguka kwa ghorofa isingefika, lakini ghorofa zinaanguka kwa sababu yanajengwa, nani achunguze, nani afanye *value* kwa sababu haijajengewa uwezo wa kifedha na utaalamu ili waweze kufanya *value for money auditing.* Ushauri wangu mimi Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri wa Fedha afisi hii waiongezee uwezo wa kifedha na kitaaluma ili watendaji wake wazidi kuikoa nchi na wazidi kutuletea mafanikio.

Mhe. Spika, jengine ningetaka niipongeze ni Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, nawapongeza sana kwa kuanzisha Kamati ya Kusimamia kesi kwa sababu kamati hii imewashirikisha wadau mbali mbali kama polisi, wanasheria na watu wengine. Mimi binafsi niipongeze kamati hii na niwaombe kwamba waendelee kushirikiana ili mrundikano wa kesi mbali mbali hapa Zanzibar uweze kupungua na waweze kutoa haki vizuri zaidi.

Mhe. Spika, jengine ambalo ningeligusia kwa ufupi ni Afisi ya Mrajis Zanzibar. Nataka niungane na Mhe. Ali Moh'd Bakari kwamba kweli Mhe. Waziri, Mrajis wa Zanzibar hana usafiri na haipendezi kuona kwamba kila siku anapanda gari yake binafsi na huku wengine wakitanua kwenye magari ya serikali ambayo ni sehemu ya nchi hii hii.

Mhe. Spika, jengine kwa kesi hii, ningetaka Mhe. Waziri atugusie lile sakata la wizi wa kompyuta kwa sababu ni utawala bora tujue tumefikia wapi. Tujue nini maamuzi ya wizara yake na tumefikia hatua gani ili tuweze kujua ni kweli utawala bora upo au ni nadharia ya utawala bora.

Jengine Mhe. Spika, ni suala zima la utayarishaji wa vyeti wilayani. Maofisi ya Wilaya Unguja na Pemba yamekuwa yakitayarisha vyeti vya kuzaliwa kwa kutumia hizi mashine za *typewriter*. Lakini mashine zile ni za zamani na

yamekuwa yakiacha baadhi ya maneno pale wanapoandika. Mtu huyo huyo anayepewa cheti kile baadae huambiwa cheti kile kimefojiwa. Sasa Mimi ushauri wangu na ningeuliza hasa, hakuna utaratibu wa kutengeneza vyeti hivi kwa kompyuta mpaka tutumie zile mashine za zamani? Kama hakuna utaratibu huo ni wajibu wa Mhe. Waziri kutafuta mashine mpya ili kuwapatia watu huko wilayani na kuondosha malalamiko.

Jengine ambalo linasumbua wananchi hasa Pemba ni ubadilishaji wa vyeti vya kuzaliwa vile vidogo, lazima vyeti vile vije Unguja. Sasa unamtoa mtu Pemba na cheti kimoja akipeleke Unguja akifuatilie ni gharama kubwa. Sasa mimi ushauri wangu ni kwamba mngewaambia utaratibu wa kukusanya kule wilayani na hatimaye wilaya iwe dhamana ya kupeleka Unguja kwa ajili ya kufanya ubadilishaji.

Lakini mwisho kabisa Mhe. Spika, niseme kwamba niwapongeze CCM kwa kuonesha kwamba wana demokrasia. Mimi nilikuwa nina wapinzani tisa lakini Urais wana wapinzani 11 hadi leo. Nawapongeza na demokrasia ikamate mkono wake. Ahsante sana

**Mhe. Najma Khalfan Juma:** Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi kwa wakati huu kuchangia machache katika wizara yetu hii tunayoipenda sana. Kwanza nakuja katika mambo ya utawala bora ule mpango uliobuniwa na Mahakama wa kutumikia jamii.

Wale wafungwa wakishapelekwa Chuo cha Mafunzo kuna mpango maalum uliotengenezwa tuone kwamba baadhi ya wafungwa waliokuwa si matata na hawana kesi kubwa wanatumikia jamii. Mpango huu ni mzuri lakini bado haujatekelezwa inavyopaswa. Mpaka sasa hivi naona ni vijana wachache tu ndio wanaoifanya kazi hii. Kwa kweli hawajapelekwa katika hiyo jamii yenyewe, wamo mle mle ndani Chuo cha Mafunzo wanatumikia.

Sasa tunataka mpango huu kama upo na umeshajaribiwa umeonekana unafaa, basi uweze kutekelezwa kwa watu wengi kwa sababu utapunguza mzigo kwa serikali ya kuwalisha wafungwa wengi mle ndani ambapo wengine wanaweza wakawa wako nje wakaitumikia jamii na jamii ikafaidika hadi muda wao utakapokwisha.

Kwa mfano, juzi takriban watu wengi humu walitokwa na machozi wakati Mhe. Zahra Ali Hamad aliposema ile kadhia inayowafika watoto kule ndani. Sasa watoto ni watoto, hawa wanaweza kufanywa nao ikiwa si watoto watukutu sana wakaweza kuitumikia jamii. Kama pana majani wakafyeka, pana mambo mengine wakafanya, kwa sababu hawa ni watoto unaweza ukawapinda. Kwa hivyo, hawa watoto nao watiwe katika *pilot area* ya

kuitumikia jamii kuliko kuwaweka ndani sana ambako wanakuwa hawajifunzi kitu kama tulivyotarajia isipokuwa maisha yao yanazidi kuharibika. Sasa kama kuna mpango huu uliopo ambao bado ni vijana wachache wanaotumikia, naomba wizara hii ifanye maarifa na hao watoto nao wawatie katika kutumikia jamii.

Halafu kuna tatizo jengine la vyeti vya kuzaliwa kisiwani Pemba. Vyeti vya kuzaliwa Kisiwani Pemba vinapatikana kwa wale wanaozaliwa leo. Lakini kuna tatizo hapa limejitokeza mwaka huu, matatizo ya vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi. Watu wazima wengi wamekosa haki yao ya kujiandikisha hasa kule kwetu vijijini Pemba kwa sababu hawana vyeti vya kuzaliwa wale wazamani.

Mhe. Spika, si wengi wenye vyeti vya kuzaliwa ni wachache mno. Kwa sababu zamani watu wanazaa lakini walikuwa hawaendi kujiandikisha vyeti, hata huyo Sheha alikuwa haarifiwi kwamba mtu kishajifungua. Hata huyo mtu aliyeandikiwa cheti ilikuwa havijawa na umuhimu mkubwa sana, hivyo wengi waliacha vile vyeti vikapotea, wengine hawakuandikishwa, sasa imekuwa shida kubwa inawapata.

Wanakwenda pale Wete penye afisi yetu kutaka hivi vyeti, mtu anatoka Micheweni, Mkoani, shamba za Wete, Chake-Chake wote wanakutana pale Wete. Lakini wanapofika pale wakishakutimiza hayo masharti wanaambiwa vyeti vile wavifuate Unguja. Sasa nasema hivi, kwa maisha ya kwetu Pemba magumu mtu ile nauli ya kutoka huko anakotoka mpaka akafika Wete basi akiondoka pale anagandwa na mfanyakazi wa pale, kwamba mimi baba nimeshakuja lakini nauli ya kurudia sina basi nauli unipe wewe, seuze nauli ya kutoka pale akaja Unguja inakuwa ni ngumu zaidi kwake yeye.

Ule utaratibu kishaufanya lakini cheti hapati kwa sababu mpaka aje Unguja. Sasa mimi ningeiomba wizara hata hawa wa zamani ambao wako kule Pemba hivi vyeti bora vingelitengenezwa na wizara hata kama wizara yenyewe ndio watakaovichukua kule Pemba wakavileta Unguja lakini halafu virejeshwe Pemba. Watu wa Pemba wakachukulie kule kule Pemba wasije huku Unguja, nauli hana mtu ya kujia Unguja. Aje Unguja kwa nauli, arudi kwa nauli japo pana jamaa zake lakini akirudi atataka zawadi japo ya mfukoni hapa Unguja sijui nini atachukua kwa sababu hapana tosi, atachukua japo chipsi au tofi hana.

Kwa hivyo, mimi naiomba wizara tusiwalazimishe watu waje huku Unguja hatuna uwezo jamani. Watu wa Pemba hawana uwezo huo hasa wa kwetu vijijini.

Mimi ningeliiomba wizara iwafanyie tahfifu hivi vyeti vikishatengenezwa pale Wete viletwe huku kiserikali, halafu virudishwe kule kiserikali, baadae waambiwe Masheha wao au watangaziwe wakachukue vyeti vyao pale Wete.

Halafu nakuja kwenye Wakfu na Mali ya Amana Pemba. Mhe. Spika, Pemba kuna wakfu mwingi sana, wengine huo wakfu wenyewe wala hawaujui. Bahati nzuri hivi karibuni tulipitisha sheria yao.

Sasa tulipopitisha sheria kidogo tumewapa meno ya kuifanya ile kazi. Kuna vijana pale wanaifanya hii kazi. Chake-Chake kuna mtoto wa kike, mimi namjua zamani sana, wazamani sana, naona nimesoma naye skuli yuko pale wakfu, anakuja mpaka *archive* huku kutafuta zile karatasi za zamani za wakfu anapata.

Mhe. Spika, akizipata anawaandikia watu waliokabidhi zile kwa sababu kuna nyumba, mashamba, milango ya maduka, lakini hizi zote ni wakfu, akishakuzijua anawaandikia wale, jamani huu ni wakfu wa fulani bin fulani. Kwa hivyo, unatakiwa wewe pesa ulete huku au tukutane turekebishane, wanapata kutishiwa mpaka maisha yao hawa. Hawa watenda kazi wa wakfu wanafanya kazi ngumu lakini wanatishiwa maisha yao, wanaandikiwa mpaka barua kwamba utakoma wewe si unajidai kutafuta wakfu?

Sasa mimi ningeiomba wizara na watu wanaohusika na mambo ya Wakfu na Mali ya Amana huko na kwa Mufti wayazungumze mambo haya sana katika vyombo vya habari. Nini umuhimu wa wakfu na nini madhara ya kwamba wewe unaujua huu ni wakfu ukaukamata kama kile kitu ni chako kumbe ni cha mtu mbali, pengine ni wakfu umewekewa Msikiti, pengine mtu mwenyewe kaandikia watoto wake. Sasa watu wanakamata hii hasa milango ya maduka.

Milango ya maduka pale Chake-Chake imekuwa ni mali kubwa kuliko hapa Unguja. Sasa hivi kutokana na huku kupelekwa umeme, imekuwa ni balaa kubwa. Chake-Chake sasa hivi kupata mlango wa duka ni shida sana, haya ndio maendeleo tuliyokuwa tunayatarajia na yashafika. Sasa kila mtu mwenye shamba ya wakfu anazuia hataki kusema kama huu ni wakfu, akiandikiwa anatishia maisha ilimradi mtafaruku wa Juma Mbaruku umepatikana tangu umeme kuingia pale kila mtu anataka adhibiti yeye.

Mimi ningeomba Mhe. Spika, wizara hii ikafanya kazi zaidi na ikawajulisha hawa watu hatari ya wakfu. Watu wanaohusika kwa Mufti kule hivi vipindi wazidi kuvibainisha kwa uwazi zaidi. Watu wa wakfu pia washirikiane na Mufti wawaeleze watu sheria za Kiislamu, nini wakfu na nini madhara ya kuzuia wakfu na hawa vijana wasitishwe waachiwe wafanye kazi yao.

Kama huyo mtoto wa kike maskini anafanya kazi yake, mtoto wa kike unamtisha vipi? Utaona wewe, ataona nini? Sasa hii kwa kweli inasikitisha. Hapa wizara inataka iingilie kwa nguvu zake zote hili, hizo wakfu izijue na izipate. Pemba ziko nyingi wakfu.

Halafu nyumba ya wakfu ya Msikiti wa Chachani aliyosema ndugu yangu Mhe. Hija Hassan Hija sasa hivi. Nyumba hii haikuishia ile ghala ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Mimi ni mtu wa Chake-Chake, nimezaliwa Chake-Chake mjini, tena nimekulia huko huko mjini napajua petu pote palivyo. Ule Msikiti haukuishia pale kwenye ghala, umeishia mpaka kwenye makontena palipojengwa duka, ukitizama utaona alama ya ukuta ipo, ile yote ni sehemu ya Msikiti ule kwa sababu ulikuwa ni Msikiti wa Shia na sisi pale ndio tuliokuwa tukikaa chini yake.

Siku ikifika *Muharram* pale tulikuwa tunakwenda tunapewa *sharbati*, tukipewa vitu chungunzima watoto. Sasa tunajua kwamba mpaka huu ukuta uliotambaa pale yote ni sehemu ya ule Msikiti. Kwa hivyo, lisifuatiwe hili ghala tu la Wizara ya Elimu, mpaka wale walioweka makontena na wengine wakajenga katika ule ukuta. Ile ni sehemu ya wakfu ya Msikiti wa Chachani.

Naomba wizara ilifuatilie suala hili na wale wajulikane vipi, watalipa au wataondoshwa? Au vyenginevyo vyovyote vifanywe lakini hii ni mali ya Msikiti, mpaka ule ukuta urejeshwe kwa sababu ile ni sehemu ya ule Msikiti si sehemu ya mtu mwengine, maana yake watu wamechukua labda kama ni sehemu ya majenzi. Ndio, ardhi ni mali ya serikali lakini huu ni wakfu. Kwa hivyo, usiishie pale penye ghala na hii sehemu iliyotiwa ukuta yote ifuatiliwe.

Wakfu mwengine ni huu Msikiti wa Mabohora pale Chake-Chake. Huu una mgogoro mkubwa, kelini wa Mabohora lakini uko chini ya wakfu sasa hivi kwa sababu hawa wenyewe hawapo na uliandikwa wakfu.

Kwa hivyo, na hili nalo lifuatiliwe, hao wafanyakazi wa wakfu Chake-Chake wanalijua vizuri suala hili. Mhe. Waziri mimi naomba ukaenao wakueleze hizi wakfu za Pemba na hawa wanaozuia na nyengine wasaidiwe na wizara kuzitafuta kwa sababu bado hizi wakfu zipo nyingi.

Mhe. Spika, nimekwambia sitokuwa na mengi lakini haya niliona bora niyabainishe kwa Mhe. Waziri ili kama kuyafuatilia na kuyatendea kazi hasa wakfu afuatilie na Mwenyezi Mungu atampa kheri na nguvu ya kufuatilia kwa sababu hili ni jambo la Waislamu na ni jambo la kidini. Ahsante Mhe. Spika.

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Najma Khalfan, majadiliano yanaendelea. Inaonekana wajumbe mmetosheka, sijui kama Mhe. Waziri yuko tayari au vipi. Naomba sasa nimkaribishe Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora.

## TAARIFA

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora:** Mhe. Spika, mimi naomba kutoa taarifa kwamba nitakuja kufanya majumuisho kwenye kipindi cha jioni.

**Mhe. Spika:** Basi sasa nikuombe utoe hoja.

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora (Kny. Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi):** Mhe. Spika, kwa kuwa Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora ameleta ombi la kwamba atafanya majumuisho wakati wa saa 11:00 jioni, naomba kutoa hoja kwamba Baraza hili liahirishwe hadi saa 11:00 jioni.

**Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii:** Mhe. Spika, naafiki.

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe ombi ndio hilo, wanaokubaliana na hoja wanyanyue mikono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

*(Saa 5:10 asubuhi Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)*
*(Saa 11:00 jioni Baraza lirudia)*

*(Majadiliano yanaendelea)*

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe tulimaliza majadiliano pale asubuhi, kwa hiyo kazi iliyobaki sasa ni kumwita Mhe. Waziri na wakati huo huo watendaji wangu watahangaika kuwapigia simu wajumbe ili waje haraka tuweze kupitisha vifungu.

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora:** Mhe. Spika, kwanza napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya na uzima nikaweza kuja tena mara ya pili katika Baraza hili kwa kutoa ufafanuzi wa hapa na pale ambao wajumbe wenzangu wa Baraza la Wawakilishi wametoa michango yao.

Mhe. Spika, michango ya Waheshimiwa Wajumbe ilikuwa mizuri sana pamoja na kuwa waliochangia walikuwa ni wachache, lakini hata hivyo waliteua mambo ya kuchangia ambayo yanaisaidia sana wizara yangu katika kufanikisha majukumu yake.

Mhe. Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuwataja watu 12 ambao wamechangia katika wizara yangu:-

1. Mhe. Haji Mkema Haji
2. Mhe. Zahra Ali Hamad
3. Mhe. Nassor Ahmed Mazrui
4. Mhe. Zakiya Omar Juma
5. Mhe. Said Ali Mbarouk
6. Mhe. Rashid Seif Suleiman
7. Mhe. Hamad Masoud Hamad
8. Mhe. Salmin Awadh Salmin
9. Mhe. Ali Moh'd Bakari
10. Mhe. Ali Abdalla Ali
11. Mhe. Hija Hassan Hija
12. Mhe. Najma Khalfan Juma

Mhe. Spika, wajumbe wote hawa walitoa mawazo mazuri sana ambayo yamesaidia sana wizara yangu. Ni kawaida ya Baraza lako Mhe. Spika, kuipa wizara yangu michango ambayo inasaidia sana kusukuma utekelezaji wa wizara hii.

Mhe. Spika, hoja zimezungumzwa nyingi sitaweza kuzifafanua moja baada ya moja, lakini nitazungumza kwa uchache tu zile ambazo nimeziweka katika maandishi ambazo nitazijibu hapa sasa hivi.

Mhe. Spika, naanza kwa mchangiaji wa kwanza ambaye ni Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Mhe. Haji Mkema Haji. Kamati imeleta hoja ya kwamba baadhi ya wakuu wa taasisi zetu kutofika mbele ya kamati.

Hii Mhe. Spika, ilikuwa bahati mbaya sana na ametaja taasisi mbili, taasisi ya Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali na Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, hii ilitokana na kuingiliana kwa ratiba za vikao, hilo ndio lilikuwa tatizo.

Lakini hata hivyo, ni vizuri maafisa wakajifunza pahala pakuweka *priority* kwenye masuala yetu haya ya utekelezaji wa majukumu yetu. Kwa hivyo, mimi naahidi kwamba nitawaelekeza wakati mnapokuwa katika kikao cha Baraza

*priority* iwekwe katika Kamati za Baraza kwa sababu ndipo panapoanza kupikwa mambo mengi ambayo wao ndio baadaye wanatakiwa wayatekeleze.

Mhe. Spika, Mhe. Makamo Mwenyekiti alitaka tahadhari ichukuliwe katika ujenzi wa jengo la afisi Pemba kutokana na hali ya ardhi ya Tibirinzi. Afisi imekutana tena na mshauri wa ujenzi na kukubaliana kufanya tathmini ya kina ya ujenzi kulingana na hali ya ardhi ya sehemu hiyo. Hii ilikuwa ni Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, pamoja na Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Afisi itaendelea kufuatilia kwa karibu zaidi suala hilo na ikihitajika itaomba kubadilishiwa kiwanja cha ujenzi. Aidha, napenda kumjulisha kwamba taratibu zinaendelea ili Mahakama ya Biashara nayo ianze kufanya kazi katika mwaka mpya wa fedha 2010/2011 kwa kupatikana kwa watendaji pamoja na vifaa vya kufanyia kazi.

Mhe. Spika, tunashukuru kwa pendekezo lake la kuendelea na ujenzi wa Mahakama ya Mkoa wa Kusini huko Tunguu ili kuongeza kasi ya kufanya kazi za Mahakama na kuondoa usumbufu wa majengo ambayo yako karibu na nyumba ya kuishi raia.

Aidha, ushauri wake wa kuondoshwa mchwa katika jengo la Mahakama ya Konde umechukuliwa na Mhe. Spika, naahidi kwamba hilo litafanyiwa kazi. Tunafanya *fumigation* pale Konde lakini sijui kama zile dawa zinakuwa zime-*expire* au vipi, lakini kila tukifanya *fumigation* haichukui muda mrefu mchwa wanarudi tena. Itabidi tuwaeleze wenzetu wa Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira kama kuna dawa ambayo pengine bei wameiweka kubwa wanaona taabu kutuambia.

Maana ilitokezea wakati mwengine wanaona taabu kutuambia tu kwamba dawa hasa nzuri hapa ni ya aina fulani lakini wakiona gharama kubwa wanakuwa hawatwambii. Mhe. Spika, tutawaomba wakubali kutuambia kwa sababu ukweli matengenezo makubwa tuliyoyafanya juzi mchwa wametuharibia sana pale katika Mahakama ya Konde.

Mhe. Spika, kuhusu kutokuwepo kwa Makadhi Wilaya ya Konde na Wete, napenda kumjulisha Mhe. Haji Mkema Haji kwamba ni kweli Kadhi wa Konde amefariki muda mrefu uliopita, Mahakama iko mbioni kujaza nafasi hiyo.

Hata hivyo, napenda kumjulisha Mhe. Haji Mkema Haji kwamba baadhi ya Mashekhe waliwahi kufanyiwa usaili ili kujaza nafasi hiyo lakini kwa bahati mbaya hakuna hata mmoja aliyefanikiwa kujaza nafasi hiyo kutokana na kutokuwa na sifa. Usaili umeshafanywa kwa ajili ya kujaza nafasi hizi lakini

ndio bahati mbaya hatujapata watu kidogo *competent* ambao wanaweza kujaza nafasi hii. Juhudi zinachukuliwa za kupatikana mtu wa kujaza nafasi hiyo. Kuhusu Kadhi wa Wete nafasi hiyo haipo tupu, bahati mbaya huyo kadhi alikuwa mgonjwa lakini sasa hivi Mwenyezi Mungu amempa nafuu na anaweza kufanya kazi zake.

Mhe. Spika, pendekezo la kuwatafuta vijana ambao wamesoma vyuo mbali mbali ili kuwa Makadhi limechukuliwa. Hata hivyo, napenda kumfahamisha Mhe. Haji Mkema Haji kwamba sifa za kielimu sio kigezo pekee ambacho kinatosha mtu achaguliwe kuwa Kadhi wa Mahakama yoyote ya Zanzibar.

Kunakuwa na sifa nyengine nyingi tu, hata tabia na mengineyo. Kwa hivyo itabidi zote hizo ziwe zinatazamwa kwa sababu unaweza ukasoma lakini tabia zako ikawa hustahiki wewe kufanya kazi ya ukadhi pale, hilo suala ni lazima liangaliwe vile vile.

Kuhusu posho la wazee wa Mahakama, napenda kumjulisha Mhe. Haji Mkema Haji kwamba hivi sasa posho hilo limeongezwa kutoka shilingi 5,000 kwa siku hadi shilingi 15,000. Hata hivyo, tatizo linalochelewesha kuwalipa wazee hao kwa wakati ni kutokana na uchache wa fedha zinazopatikana kutoka serikalini.

Mhe. Spika, hili suala la fedha kwa ajili ya Mahakama, Serikali inalifanyia kazi sana. Ni lazima Mahakamani tu-*allocate* pesa za kutosha sana ili hizi kesi ziweze kusikilizwa kwa wakati. Nina hakika mheshimiwa anayehusika na masuala ya fedha hii hali anaijua na ameahidi kwamba hilo suala litarekebishwa katika mwaka unaofuatia. *(Makofi).*

Mhe. Spika, afisi itaangalia uwezekano wa kuongeza ada ya ukaguzi kwa taasisi za serikali kwa ajili ya kuongeza mchango wake katika mfuko mkuu wa serikali. Aidha, afisi imeweza kufikia lengo la kukusanya mapato kwa mwaka wa fedha 2009/2010 kwa asilimia 100 kutokana na bajeti iliyopangwa na afisi. Hili lilikuwa ni suala la Afisi ya *CAG*, yaani Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Aidha, afisi itahakikisha hatua muafaka zitachukuliwa dhidi ya wale ambao ni wagumu kulipa ada za ukaguzi.

Hata tulipokuwa katika kamati kule walisema kwamba itakuwaje leo mashirika yanafanya biashara yashindwe kulipa ada ya pesa ambazo ni chache sana. Wakapendekeza kwamba hata ikibidi basi ni vizuri mashirika hayo yafungwe na katika hotuba yake ameeleza hivyo hivyo kwamba mashirika hayo kama ikiwa ndio kweli wanafanya biashara lakini wanaona taabu kulipa basi yafungwe.

Mhe. Spika, mheshimiwa alizungumzia juu ya suala la hutoba aliyoisikia Ijumaa iliyopita katika Msikiti wa *Wireless* ambapo *Khatib* alizungumza juu ya Baraza la Wawakilishi kupitisha Mswada wa Haki ya Mtoto wa Kizanzibari na kwamba kila aliyeshiriki kuupitisha mswada huo ni dhalim.

Mhe. Spika, huu mswada bado haujapitishwa uko katika mchakato. Kwa kweli mimi nasema kwamba wale walionao mswada wamefanya jambo zuri sana kuupitisha kwa wadau kabla ya kufanya maamuzi ya kuuleta kwenye Baraza. Sasa nafikiri wao wataanza kupata habari kwamba wadau wanasemaje kuhusu suala hili. Hizo habari watazipata sasa hivi kwa sababu hilo suala limeshazungumzwa katika vikao vingi. *(Makofi).*

Mhe. Spika, wizara yangu kupitia kwa viongozi mbali mbali wa dini mara nyingi imekemea tabia ya baadhi ya Maimamu na Makhatib Msikitini hukurupuka na kuzungumza mambo ambayo hawana uhakika nayo. Qur-ani inatufundisha Waislamu kutolizungumza jambo unalolisikia au kulichukulia hatua bila ya kulifanyia uchunguzi wa uhakika. Juhudi za kuwaelimisha viongozi wa dini juu ya umuhimu wa jambo hili zitaendelea. *(Makofi).*

Mhe. Spika, mjumbe mwengine ni aliyemwakilisha Waziri Kivuli, Mhe. Zahra Ali Hamad. Alieleza kwamba kuna kasi ndogo ya upelekaji waendesha mashtaka wa kiraia katika Mahakama za Wilaya na kutoka mwaka huu wilaya zote zipate waendesha mashtaka wa kiraia.

Mhe. Spika, hiyo jitihada inafanywa na ili kupeleka waendesha mashtaka katika ngazi ya wilaya mambo kadhaa yanahitajika. Moja kuwaajiri wanasheria na kuwapatia mafunzo ya angalau miezi sita ya uendeshaji wa mashtaka. Pili kupata afisi na vitendea kazi katika hizo sehemu wanazopelekwa. Tatu kupata usafiri kwa ajili ya kufuatilia mambo kadhaa ikiwemo kukutana na wapelelezi, maeneo ya uhalifu, mashahidi na kadhalika. Hivi ndivyo inavyopeleka Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka hawa watu waendesha mashtaka katika maeneo.

Hii kwa wale walioko Pemba nafikiri wataona mifano kwamba katika zile sehemu ambazo kwa bahati hawana afisi wamejenga wenyewe, Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka wanajenga afisi kabisa. Wamejenga Mkoani pale chumba wamekifanyia matengenezo, Wete chumba wamekifanyia matengenezo kwa ajili ya kuwawezesha kufanya kazi hizi. Sasa hivi wana mpango vile vile wa kuona kwamba na Chake-Chake napo wanajenga chumba cha kufanyia kazi hizi. Hii ni lazima kwa sababu wale waendesha mashtaka wapate pahala ambapo watafikia kabla ya kwenda katika chumba cha Mahakama.

Mhe. Spika, afisi ilikuwa na lengo la kukamilisha kupeleka waendesha mashtaka katika Mahakama zote za wilaya mwishoni mwa mwaka huu. Hata hivyo, kutokana na kuingizwa fedha kidogo kulingana na mahitaji, afisi itashindwa kupeleka waendesha mashtaka wa kiraia kwa mwaka huu katika Mahakama za Wilaya Mkokotoni na Makunduchi kwa Unguja na Mkoani na Konde kwa Pemba. Pamoja na kuwa vyumba vile viko kule lakini tatizo hili lipo. Konde hawajamaliza kile chumba ambacho wanataka kukitumia lakini wameanza kukijenga.

Mhe. Spika, afisi iliomba kuongezewa shilingi 240,000,000 kwa ajili ya matumizi mengineyo na mishahara lakini fedha zilizoongezwa ni shilingi 14,000,000 ambazo ziliongezwa kwenye mishahara. Kwa hivyo, kwa mwaka huu afisi itapeleka wanasheria katika Mahakama za Wilaya zilizopo Mwera na Mfenesini kwa Unguja, Chake-Chake na Wete kwa Pemba. Ni matarajio ya afisi kwamba serikali itapata uwezo wa kukimu gharama hizo katika mwaka wa fedha 2011/2012.

Mhe. Spika, napenda kumjibu Mhe. Waziri Kivuli kwamba Waheshimiwa Majaji, Mahakimu na Makadhi wako chini ya Tume ya Utumishi wa Mahakama ambayo moja ya kazi yake kubwa ni kupendekeza kwa serikali maslahi ya watumishi hao. Tume ilipendekeza viwango vya mishahara kwa nia ya kuongeza maslahi yao, lakini mapendekezo hayo hayakukubaliwa kutokana na uhaba wa fedha. Hali tofauti ya viwango vya mishahara baina ya Mahakimu, Makadhi wenye elimu sawa inasababishwa na ngazi, uzoefu wa kazi pamoja na majukumu.

Kwa mujibu wa sheria za Zanzibar nafasi ya Mrajis wa Mahakama au Naibu wake haikuelezwa sifa za kielimu ili mtu aweze kushika nafasi hiyo kama ilivyo kwa majaji, mahakimu na watendaji wengine. Kwa maana hiyo Naibu Mrajis wa Mahakama Kuu kiutawala na kiutendaji yeye ana madaraka na majukumu mengi na makubwa kuliko mahakimu. Hivyo basi mshahara wake unatofautiana na mahakimu.

Mhe. Spika, kuhusu kuanzishwa kwa Mahakama ya Ardhi kwenye mikoa ya Zanzibar ushauri huo unachukuliwa. Lakini napenda kumfahamisha mheshimiwa kwamba kiutawala Mahakama ya Ardhi haiko chini ya utawala wa Mahakama Kuu. Mahakama ya Ardhi iko chini ya wizara inayohusika na mambo ya ardhi, yaani Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi. Sisi tunawasaidia kuwapatia hao mahakimu tu lakini iko kwao. Hata hivyo, ushauri uliotolewa na Waziri Kivuli unachukuliwa na kufanyiwa kazi.

Mhe. Spika, kuhusu kufanya ukaguzi kuzingatia viwango vya kimataifa afisi imeshachukua hatua ya kuanzisha Muongozo wa Ukaguzi *(Regulatory Audit*

*Manual)* ambao unakubalika kitaifa na kimataifa pamoja na kufuata sheria na kanuni za ukaguzi zilizotolewa na Jumuiya za Kimataifa za Ukaguzi *(INTOSAI).* Muongozo huu unaanza kutumika hivi karibuni.

Mhe. Spika, Waziri Kivuli alizungumzia masuala mawili makubwa ikiwa ni pamoja na ongezeko la mabaa katika manispaa ya Zanzibar.

Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Zahra Ali Hamad juu ya ongezeko kubwa la mabaa katika maeneo mbali mbali hapa nchini. Wizara yangu kupitia kwa Afisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar imekuwa ikichukua juhudi za makusudi kuwaelimisha Waumini kwa jumla juu ya uharamu wa biashara hii na madhara yake kwa jamii. Pia tunawahimiza wananchi kwa jumla watumie haki yao waliyopewa ya kupinga kuanzishwa kwa mabaa katika maeneo yao.

Ninayo taarifa juu ya juhudi mbali mbali zinazochukuliwa na vikundi mbali mbali vya dini katika kuelimisha na kushajiisha Waumini juu ya kupinga kuwepo kwa mabaa katika maeneo yao. Mhe. Zahra pia alizungumzia juu ya Mswada wa Haki ya Mtoto suala ambalo liliguswa pia na Mhe. Haji Mkema Haji, Mhe. Said Ali Mbarouk, Mhe. Rashid Seif Suleiman, Ali Moh'd Bakari na wengineo ambayo nimetoa maelezo yake kwamba hilo suala liko kwenye mchakato.

Mhe. Spika, serikali katika suala la kupunguza mabaa katika mji imepandisha sana ada ya leseni na imepandisha sana kodi lakini bado watu wanajichomoza kwa kuanzisha vitu kama hivi. Maana kwa hapa mjini Mhe. Spika, ukitaka kuanzisha baa leseni yake ni shilingi milioni moja, watu wanaota shilingi milioni moja waanzishe baa.

Kila mwezi wanatakiwa walipe ada ya shilingi laki tatu, watu wanalipa hizo laki tatu kwa kuanzisha baa. Unajua haya mambo ya shetani Mhe. Spika, yana nguvu sana lakini ni vizuri wananchi nao wakatumia ile nafasi yao waliyowekewa katika ile sheria ya kutoa malalamiko kwamba hapa petu hapastahiki kuwa na baa.

Hii imefanywa kwa sababu ilikuwepo baa ikiitwa *Bottom Up* imefungwa kwa sababu wananchi waliilalamikia. Kuna Jozani pale Miembeni imefungwa, kuna Jitini pale Miembeni imefungwa. Mhe. Spika, ilikuwa balaa huwezi kupita pale usiku kabisa, utaona mambo ambayo hutaki kuyaona lakini itabidi uyatazame. Hali ilikuwa mbaya sana pale lakini kwa sababu wananchi wamelalamika *Alhamdulillahi* zile baa zimefungwa na sasa hivi mambo shwari pale.

**Mhe. Spika:** Bahati nzuri sikuwahi kupita hata siku moja.

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora:** Mhe. Spika, bahati nzuri sana kama hukupita pale lakini ingekuwa balaa.

Mhe. Spika, Mhe. Zakiya Omar Juma lakini kwanza nianze na Mhe. Nassor Ahmed Mazrui ambaye naye ndiye alifungua dimba katika wachangiaji. Mhe. Spika, Mhe. Mazrui alifanya jambo moja jipya na ni zuri nimelipenda. Kwanza alitoa mchango muda ulipomalizika ulimwambia akae kitako, akakaa kitako lakini akaleta mchango wa maandishi, maana hakumaliza mchango wake. Kwa hivyo, nampongeza sana kwa hili. Ni njia nzuri kabisa ya mtu kukamilisha mchango anaotaka kuutoa na nitaeleza mchango aliouleta.

Mhe. Spika, kwanza katika *platform* ile alizungumzia masuala ya Mahakama ya Biashara itaanzishwa lini. Mhe. Spika, Mahakama ya Biashara itaanzishwa kwenye mwaka huu tunaopitisha bajeti yake. Jengo tumeshalipata na tumeshalifanyia matengenezo lililokuwa Maktaba Kuu. Kwa hivyo pale ndio tutaanza Mahakama ya Biashara.

Halafu alizungumza kazi ya kuimarisha mazingira ya biashara. Hii kazi Mhe. Spika, imeshaanza na tunakwenda na *inshaallah* tunategemea kwamba tutafanikiwa Mwenyezi Mungu akitujaalia.

Katika hili Mhe. Spika, kuna vitu maalum katika kuimarisha mazingira ya biashara lazima viwepo. Kwanza Bodi ya Rufaa ya Kodi, yaani tayari hiyo bodi imeshaanzishwa ambayo watu wanaotozwa kodi wanaweza wakenda wakakata rufaa katika bodi hiyo. Mahakama ya Biashara ndio hiyo tunayosema kwamba kwenye bajeti hii tutaianzisha vile vile. Halafu *Business Council* Mhe. Spika, inasaidia sana kwenye masuala haya na wameshafanya mikutano mfululizo hapa kuzungumzia masuala mbali mbali yanayohusu uchumi na biashara kwa jumla.

Halafu kuna *Chamber of Commerce* ambayo nayo imeshabadilisha uongozi wake kwa sababu nao sasa wameshaamua kufanya kazi kweli kweli kwenye masuala ya biashara, na Mhe. Rais mara ya mwisho alipokutana nao aliwahimiza kwamba na wao waingie katika kuanzisha miradi wakiwa wananchi wa nchi hii, wasingojee tu kwamba mpaka watokee wageni kuja kuanzisha miradi hiyo.

Mhe. Spika, Mhe. Nassor Ahmed Mazrui amezungumzia juu ya ujenzi wa Mahakama kuwa za kisasa. Mhe. Spika, mimi nalishukuru sana Baraza lako tukufu limekuwa likipiga kelele sana juu ya suala hili. *Alhamdulillahi* Mwenyezi Mungu ametujaalia hata watu wa Mahakama wamesikia na Wizara ya Fedha imesikia, ndio maana Mahakama sasa hivi imeshaezekwa na mle ndani mnafanywa marekebisho.

Hivi sasa Mhe. Spika, Jaji Mkuu katika lile jengo la Mahakama hayumo mle ametoka na ameingia kwa muda katika lile jengo linalotaka kutumika kama ni Mahakama ya Biashara. Hii ni kwa sababu kule kunafanywa mabadiliko ili mtu akiingia kwenye ofisi ya Jaji Mkuu ajue kwamba kaingia kwenye ofisi yenye hadhi ya kufanyiwa kazi na Jaji Mkuu. Hiyo kazi tayari inaendelea. Halafu tutafanya jitihada ya kuitanua ile Mahakama kwa kuhamisha pale Afisi ya Mahakama ya Mkoa na kujenga pahala pengine ambapo Mahakama itakuwa na nafasi kutokana na ongezeko la watu.

Mhe. Spika, mambo ambayo ameleta Mhe. Nassor Ahmed Mazrui katika mchango wake amenieleza juu ya suala la tatizo la *traffic* njiani. Anasema katika alimotembea ameona kwamba *traffic* akimkamata mtu kapanda baiskeli haina taa au breki, au kafanya kosa la ki-*traffic*, basi yule *traffic* huwa anampa karatasi maalum yule aliyemshtaki anamwambia peleka Manispaa uende ukalipe faini yako kiasi kadhaa. Hii inaepusha yule *traffic* kumtoza pesa pale na pengine asimuandikie risiti. Mhe. Spika, huu ni utaratibu mzuri na nimeupenda sana ambao Mhe. Mazrui ameueleza.

Sasa akifika kule *traffic* kama hakwenda kulipa Manispaa basi siku anayokwenda kukata leseni yake kama *road licence* au kitu chengine chochote, kompyuta inaeleza kwamba yeye alikwishapewa *notice* zile mara mbili au tatu hakulipa, kwa hivyo hapewi leseni mpaka alipe deni lote lile ambalo lililomkabili.

Mhe. Spika, hili nalikubali ni wazo zuri kabisa na itabidi tuwashauri wenzetu. Sisi ni Utawala Bora itabidi tuwashauri wenzetu wanaohusika na masuala ya *traffic*. Kwa sababu kweli kama utawapa risiti majiani nadhani mara nyingi watakuwa hawaziandiki hizo risiti zitakuwa pesa zinaingia mfukoni. Lakini kama wanaambiwa nendeni mkalipe pahala fulani hiyo itakuwa nzuri.

Halafu Mhe. Spika, kuhusu suala la jengo la Mrajis wa Serikali jitihada tunaendelea nayo. Ni kweli lile jengo liliopo sasa hivi haliwezi kuchukua vitu vya kisasa hivi. Ndio maana Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imehama pale na kukodi jengo sasa hivi la muda la Idara ya Bandari, lakini pia imenunua nyumba pale pale pembeni ya bandari na sasa inalifanyia matengenezo ili liwe ndio ofisi yake ya kudumu badala ya kulipa kodi kule kwenye jengo la bandari.

Sasa na huyu vile vile kitafutwe kiwanja akajenge. Lakini tunafikiria kwamba huyu tunazungumza na watu wa Idara ya Takwimu kwamba wana kiwanja pale Mombasa basi washirikiane katika kujenga, sehemu ya jengo lile iwe ni sehemu yao, wao watu wa Takwimu na sehemu nyengine iwe ni sehemu ya Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali.

Mhe. Spika, nakwenda kwa Mhe. Zakiya Omar Juma ambaye aliuliza kuhusiana na jalada la kutoroshwa yaliyopelekwa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, kama kuna jalada la kesi ya kumtorosha mtoto Maryam Farid. Pia alitaka kujua kuhusiana na hatua zilizochukuliwa kuhusiana na udhibiti wa madawa ya kulevya.

Katika jalada la kutoroshwa yaliyoletwa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, hakuna jalada lenye jina la Maryam Farid. Hata hivyo, tunaomba Mhe. Mwakilishi atupatie maelezo zaidi kuhusiana na kesi hiyo kama mwaka na kituo kilichoripotiwa tukio hilo ili tuweze kufuatilia. Kuhusiana na udhibiti wa matumizi ya madawa ya kulevya, Baraza hili tukufu limetunga sheria mpya ya madawa ya kulevya, Sheria Nam. 9 ya mwaka 2009. Sheria hii imeshaanza kutumika na hatua zaidi zinachukuliwa kuitungia kanuni ili kuiimarisha iweze kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.

Hapa Mhe. Spika, naomba kuwaomba Wajumbe wa Baraza lako tukufu, sheria hii itakapokuwa inafanya kazi kamili tafadhali wawe wastahamilivu sana, maana wajumbe wameizungumza vizuri sana hii sheria. Hii sheria kuna kifungu ndani yake kinasema kwamba utakapomkuta kijana anadorora pahala na ukamdhania kwamba pengine anadorora kwa sababu ya kutumia madawa ya kulevya, basi moja kwa moja umchukue umpeleke akafanyiwe uchunguzi. Akachunguzwe choo kidogo na kama kitaonekana *positive* basi huyo moja kwa moja apelekwe Chuo cha Mafunzo kwa muda wa miezi sita na akitoka huko apelekwe *Rehabilitation Centre;* yaani Kituo cha Kurekebisha Tabia.

Hii itatugusa wengi. Kwa hivyo, nadhani kwa sababu tutakuwa tunarekebisha tabia, nafikiri itabidi wajumbe tuje kuwa wastahamilivu sana wakati wa utekelezaji huo. Halafu na vifungu vyengine vikubwa vya kuwakamata watu wakubwa wakubwa ambao wanafanya biashara hii pia vimo katika sheria hii. Kwa hivyo, hiyo vile vile tusije kukubali kutumiwa katika suala la kuwaombea na mambo mengineyo ijapokuwa watu wana mbinu nyingi kabisa. Maana hili suala lazima Mhe. Spika, tulipige vita liondoke kweli kweli.

Hivi sasa kamati inayohusika na masuala haya inakutana mara kwa mara chini ya uongozi wa Mhe. Waziri Kiongozi kuzungumzia mbinu mbali mbali. Ndio maana juzi hapa Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake naWatoto akasema kwamba hata kimetayarishwa choo maalum pale Uwanja wa Ndege kwa ajili ya kuweza kuchekecha masuala haya ya watu wanaokuja na madawa ya kulevya. Pia kuna nyumba pale inafanyiwa matengenezo kwa ajili ya kuwa Polisi isitoke mbali na pale, inayohusika na masuala haya ya madawa ya kulevya. Hii jitihada inachukuliwa nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wawe wastahamilivu na *inshaallah* mambo haya yatashughulikiwa vizuri sana.

Mhe. Spika, Mhe. Zakiya Omar Juma asishtuke tukimwambia kwamba hatukupata jalada lenyewe la Maryam Farid. Tumepata jalada lenye jina la Maryam lakini sio Maryam Farid ni Maryam mwengine ambalo mpaka sasa hivi polisi wameshamaliza upelelezi na kwa muda si mrefu wametwambia kwamba watalileta kwenye Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka. Kwa hivyo, hapo ndio tutakapojua hatima ya kesi hiyo. Yumo mtoto katoroshwa naye ni Maryam lakini sio Maryam Farid. Hilo wameshamaliza upelelezi wote na watalileta kwenye Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka.

Mhe. Spika, Mhe. Zakiya Omar Juma pia alizungumzia juu ya ongezeko la mabaa suala ambalo limekwishajibiwa, ama juu ya ukahaba pamoja na mmong'onyoko wa maadili tunakiri kuwepo kwa mambo haya. Majanga yote haya yamesababishwa zaidi na wazazi kukwepa wajibu wao wa kuwalea watoto kwa mujibu wa miongozo ya dini yetu.

Mhe. Spika, polisi wanafanya operesheni ya kuwakamata hawa makahaba na kuwafikisha katika vituo kwa ajili ya kesi za uzururaji. Lakini Mhe. Spika, niseme wanapokamatwa hawa tusiwaombee kwa sababu na hili nalo linarejesha nyuma utekelezaji.

Mhe. Spika, wakifika kule wanashughulikiwa, maana wenyewe wanajibu bila ya wasi wasi, sisi tuna watu wetu hapa Unguja watakuja kutuombea, sasa hao watu wanakuja kuombewa usije ukawaona Mhe. Spika. Mhe. Spika, kwa njia hiyo tu tutawapunguza hao watu wanaokuja kufanya ukahaba hapa visiwani, ikiwa tutaacha kwamba serikali itekeleze wajibu wake juu ya masuala haya.

Mhe. Spika, Afisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar haina mashirikiano na *Jumuiya Islamic Research Center*, lakini ina mashirikiano makubwa na taasisi nyengine za kidini ambazo pia zinajihusisha na tafiti za Kiislamu. Mfano wa taasisi hizo ni:- *World Islamic Call Society ya Libya*, Afisi ya Mufti Mkuu wa Oman, Chuo Kikuu cha Azhar cha Misri nakadhalika. Lakini tutaangalia uwezekano wa kuanzisha uhusiano na taasisi hii. Hii ndio ile taasisi inayotangaza ile *Peace TV*.

Mhe. Spika, Mhe. Said Ali Mbarouk, alieleza kuwa kuna mapungufu kwenye Maabara ya Mkemia pamoja na kueleza kuwa ukosefu wa mashine ya *DNA* kunaathiri upatikanaji wa haki.

Mhe. Spika, nakubaliana na maelezo ya Mhe. Mwakilishi kuwa tatizo la kukosekana mashine ya *DNA* pamoja na mapungufu ya Maabara ya Mkemia yanaathiri upatikanaji wa haki katika kesi za jinai. Hata hivyo, wizara yangu itaendelea kuwasiliana na wizara inayohusika kufuatilia mambo hayo ili kuimarisha usimamiaji wa kesi za jinai, ili Afisi ya *DDP* kutekeleza majukumu

yake. Mhe. Spika, ushauri wa Mhe. Said Ali Mbarouk wa kuongeza kasi ya usikilizaji wa kesi umechukuliwa, lakini hata hivyo ili utoaji wa maamuzi ya kesi yoyote ufanikiwe kunahitajika kupatikana kwa mambo mbali mbali kama vile fedha, upatikanaji wa mashahidi, ukamilishaji wa upelelezi unaofanywa na jeshi la polisi n.k.

Hili ni jambo la kushirikiana na vyombo vingi kabisa. Kwa hivyo, huu ushauri tunaupokea na ninamuahidi kwamba tutaendelea kufanya mashirikiano nao.

Mhe. Spika, kuhusu ushiriki wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu katika utayarishaji wa Kanuni, kikawaida wizara na taasisi inayohusika huwa inatayarisha maeneo ambayo kwa mujibu wa sheria husika yanahitaji kutungiwa kanuni.

Hapo inaombwa Afisi ya Mwanasheria Mkuu kuyapitia maeneo hayo na kuyatungia kanuni kulingana na matakwa ya Sheria husika.
Aidha, njia nyengine ni wizara au taasisi kuandaa kanuni kwa mujibu wa sheria husika na kuwasilishwa Afisi ya Mwanasheria Mkuu kwa mapitio na kuhakiki kama kanuni hizo zimefuata matakwa ya sheria. Kuchelewa kutungwa kanuni hakutokani na Afisi ya Mwanasheria Mkuu bali inatokana na utayari wa Waziri wa Wizara na taasisi inayohusika. Kwa kuwa tupo mawaziri hapa tumeshasikia sote, nafikiri ni vizuri kila sheria inayotungwa itungiwe kanuni kwa haraka ili iweze kufanyakazi yake vizuri.

Mhe. Spika, Mhe. Said Ali Mbarouk na Mhe. Hija Hassan Hija, walishauri kuwepo kwa ukaguzi yakinifu. Afisi imejitayarisha kufanya ukaguzi yakinifu ambapo tayari imeanza kufanya mafunzo ya awali ikiwa ni hatua ya kujitayarisha. Aidha, ukaguzi huu unahitaji wataalamu wa fani mbali mbali ikiwemo wahandisi, wafamasia na taaluma nyengine.

Mhe. Spika, *value for money auditing* sio tu upeleke watu kukagua lakini na wewe mwenyewe uwe unamiliki ma-*engineers.* Kama ni jengo waweze kulitizama jengo kwamba linakwenda kwa taratibu, mchanganyo wake wa mawe, kokoto, mchanga na saruji ni wa kitaalamu.

Nondo yake inayotumika ni ya kitaalamu, vyenginevyo tutapata matatizo ya majumba yetu kuwa mabovu. Kwa hivyo, *value for money* kweli itakosekana, kama mfano alioutoa yeye katika jengo lile la Chake-Chake la Wizara ya Fedha. Sasa afisi hii inajitayarisha kufanya huo uajiri wa wataalamu waliofanikiwa katika mambo hayo pamoja na wana famasia ili kuweza kuchunguza vizuri utendaji wa kazi.

Vile vile Mhe Said Ali Mbarouk alisema ili ukaguzi huu ufanikiwe kunahitajika kuajiri watendaji wa fani hizo. Hatua za uajiri wa watendaji hao pamoja na mafunzo ya ziada yatachukuliwa katika mwaka wa fedha unaofuata, yaani huu tunaopitisha bajeti leo.

Mhe. Hamad Masoud alizungumzia juu ya Jumuiya za Dini zimekuwa na mchango mkubwa katika shughuli mbali mbali za kijamii. Kati ya vyuo vikuu vitatu vilivyopo Zanzibar, vyuo viwili vinamilikiwa na Jumuia za Dini ambazo ni *African Muslim Agency* na *Darul - Imani*. Aidha, Jumuia za Kidini zina vituo vya mayatima na vimekuwa mstari wa mbele katika kutoa misaada ya kibinadamu, afya, huduma za visima, kujenga misikiti, madrasa nakalidhalika:-

- Ili kuunga mkono juhudi zao na kwa vile mizigo wanayoileta au wanayosaidiwa huwa sio ya biashara ndio maana wanaombewa misamaha ya ushuru, kama alivyouliza Mhe. Hamad Masoud. Hawa anaofanya shughuli hizi ndio wanaoombewa misamaha;
- Jumuiya hizo zinaombewa na Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana kwa sababu kisheria ndio inayohusiana na misaada ya Kiislamu. Aidha, Afisi ya Mufti nayo huombea misaada taasisi za pamoja kati ya Waislamu na Wakristo;
- Misamaha inayoombwa imetolewa kwa zile taasisi zote zilizotimiza taratibu zinazotakiwa; na
- Kamisheni ya Wakfu pamoja na Bodi ya Mapato hufuatilia kwa karibu kuhakikisha kuwa misaada inayosamehewa ushuru inawafikia walengwa. Hiyo ndio kazi inayofanywa na Afisi ya Mufti.

Mhe. Spika, Mhe. Ali Abdalla Ali amesema miongoni mwa majukumu ya kamisheni ni kushughulikia misaada ya heri. Tumeeleza katika hotuba yetu. Kamisheni imekuwa ikijitahidi kwa kushirikiana na taasisi mbali mbali kusaidia mayatima tokea kuomba kuwatambua na mambo mengineyo. Kiutaratibu shughuli za kulea na kufungua vituo vya mayatima katika serikali hufanywa na Idara ya Ustawi wa Jamii. Hivyo, hata taasisi za kidini zinazofanya shughuli za mayatima, hufuata kanuni za Idara ya Ustawi wa Jamii pamoja na kuzingatia sheria za dini.

Mhe. Spika, sambamba na hilo tunashukuru maelekezo na ushauri uliotolewa na Mhe. Najma Khalfan juu ya kuzidi kuzifuatilia mali zilizoekwa Wakfu pamoja na maeneo yake na kwamba Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana itashirikiana na taasisi nyengine kutoa elimu zaidi kwa wananchi, juu ya umuhimu wa kuzirejesha mali za Wakfu walizozihodhi kinyume ya utaratibu kwa njia moja au nyengine.

Mhe. Spika, ni kweli kama alivyosema Mhe. Najma Khalfan kuwa wale vijana wanaofanya kazi hii hutishiwa mpaka maisha. Lakini hata hivyo tunashukuru kwamba tumeshawahi kuzipata baadhi ya mali za yatima na wengine wameandikiwa barua na wale wakirudi basi afisi huwa inafanya jitihada ya kuwaona wahusika ili warejeshe mali ya yatima.

Mhe. Spika, kuhusu hili pendekezo la kutoa elimu ni zuri sana na tutaendelea kutoa. Niliwahi kusema siku moja hapa kwamba ni hatari sana kutumia mali ya yatima. Hasa kutumia Wakfu basi ni hatari sana. Mhe. Spika, **a**idha, namshukuru Mhe. Ali Abdalla Ali na tutawasiliana naye ili kupatikana kiwanja katika eneo la Mfenesini kwa ajili ya ujenzi wa Mahakama mpya ya Mfenesini. Mahakimu hali ikiruhusu ya kifedha watapatiwa vipando.

Kuhusu uozeshwaji unaofanywa na Makadhi, kama alivyozungumza Sheikh Ali Abdalla Ali hapa badala ya Mawalii, tutawaelimisha Makadhi hao kufuata vizuri miongozo na taratibu za dini. Makadhi ni binadamu, kwa hivyo ni vizuri vile vile kila mara nao wanatakiwa wawe wanakumbushwa.

Mhe. Spika, kuhusu shamba la Wakfu la Mfenesini na Mamlaka ya Maji, ambapo Mamlaka imejenga visima na inahitaji eneo zaidi kwa matumizi yao. Hadi sasa mazungumzo yanaendelea juu ya suala hili. Aliuliza kwenye hili shamba halina tatizo lolote. Tatizo liko baina ya Idara ya Maji na Wakfu yenyewe kwamba wanataka kuongeza zaidi lazima mapatano yawepo juu ya suala hili. Pamoja na kuwa limehudumia wananchi lakini mali ya Wakfu ni mali yenye kazi maalum, kwa hivyo lazima tufike mahala tukubaliane.

Mhe. Spika, vile vile Kamisheni ya Wakfu Pemba inaendelea kufuatilia zaidi eneo la Wakfu liliopo baada ya ghala hiyo na maeneo mengine ye Wakfu yanayojitokeza. Sambamba na ufuatiliaji wa nyakfu mbali mbali, Kamisheni imo katika mchakato wa kutafuta nyaraka za asili za Msikiti uliopo Chake-Chake uliotumiwa na Waumini wa Isnath-shiria, yaani ni Msikiti wa Mabohora ambao Mhe. Najma Khalfan ameutaja. Msikiti huu unaendelea kufuatiliwa kupata nyaraka, mpaka sasa hivi hatujazipata nyaraka sahihi kwenye Msikiti huo.

Mhe. Spika, ni kweli kwamba upo ushahidi kwamba hapo nyuma ulikuwa ukilipwa kwenye Wakfu na Mali ya Amana, lakini sasa hivi imesita na inabidi tuwasiliane zaidi juu ya masuala haya.

Mhe. Spika, ni kweli kumekuwepo na ongezeko la maasi katika jamii na jitihada kubwa zinachukuliwa katika kuelimisha waumini juu ya umuhimu wa kumcha Mwenyezi Mungu. Hivi sasa Afisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar imo katika mchakato wa kuandaa semina kwa waumini wa mikoa yote ya Zanzibar,

kuhimiza juu ya ucha-Mungu na umuhimu wa amani na utulivu nchini, hasa katika kipindi hiki cha kuelekea katika uchaguzi mkuu. Mhe. Mazrui masuala yako nimeshayajibu lakini yapo masuala machache kidogo yanayomuhusu Mhe. Hamad Masoud ambayo anazungumzia kuhusu masuala ya Mahakama kwamba kesi ikimalizika dhamana ya fedha hutakiwa kurejeshwa kwa aliyeweka.

Moja ya tatizo linalochelewesha urejeshaji wa dhamana hizo ni utaratibu wa kuzitoa kutoka Hazina, kwani fedha za dhamana hazihifadhiwi kwenye tajuri la Mahakama bali huhifadhiwa Hazina, na inapotokea kesi kumalizika huombwa huko kwa ajili ya kumrejeshea aliyeweka. Nafikiri urasimu wa Hazina Mhe. Hamad Masoud anaujua vizuri sana, hata na yeye anapopata tenda za ujenzi nafikiri huona hiyo hali inayompelekea katika kutafuta pesa zake.

Mhe. Spika, kuhusu uteuzi wa Majaji wa Mahakama Kuu. Napenda kumjuilisha kwamba uteuzi huo hufanywa kwa kuzingatia matakwa yaliyowekwa na Katiba ya Zanzibar ya 1984. Hata hivyo uzoefu tu wa uwanasheria katika taasisi sio kigezo pekee cha mtu kuweza kuteuliwa kuwa Jaji wa Mahakama Kuu. Hivyo kunapotokea kujazwa kwa nafasi tupu ya Jaji wa Mahakama Kuu hutafutwa mtu ambaye ana sifa za kupendekezwa na Mhe. Rais wa Zanzibar ili kumteua.

Mhe. Najma Khalfan umezungumzia suala la watoto. Kama alivyozungumza Mhe. Zahra katika kikao kilichopita. Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ alisema juzi. Bila shaka lile jibu alipata kutoka kwa watu wa Mahakama kwamba sasa watatenga eneo maalum pale kwenye gereza kwa ajili ya kuwaweka watoto na itakuwa hakuna ruhusa ya kuingia mtu yeyote. Lakini hata hivyo wakati huo wanafanya jitihada za kuhamisha kile kituo ili wajenge mahala peke yake kama ni Mahakama ya Watoto, na isiwe karibu na kile Chuo cha Mafunzo kilichopo hivi sasa hivi. Mlimsikia Mhe. Waziri jana alijibu na hiyo ndio jitihada itakayotokea.

Mhe. Spika, Mhe Rashid Seif Suleiman amezungumzia suala la Idara ya Uratibu kufanya tathmini ya kujua taasisi za serikali zimetekeleza vipi suala la utawala bora.

Mhe. Spika, idara bado haijafanya tathmini kwa sasa ila imo katika hatua za kuunda miundo mbinu ya kufanya tathmini hiyo. Kwa sasa tayari watendaji wa Idara wameshajengewa uwezo wa kufanya kazi hiyo na tayari kwa wakati huu harakati za kuanzisha kamati za kitaasisi za utawala bora zinaendelea, ambapo tarehe 31 Mei kulifanyika kikao cha awali cha kuunda kamati hizo. Lakini pia tayari kazi ya kutayarisha viashiria vya utawala bora inaendelea na tarehe 20 Julai kutafanyika kikao cha pili kuijadili rasimu ya viashiria hivyo.

Mhe. Spika, ni matumaini yetu kwamba katika mwaka wa fedha 2010/11 tutaweza kuandaa ripoti za utawala bora. Wizara inajenga mahusiano yake na taasisi za serikali na zile zisizokuwa za serikali kupitia uenyekiti wa klasta ya tatu ya MKUZA ambapo ina wajumbe wasiopungua 25. Kwa ufupi kinachoelezwa ni kwamba katika MKUZA, katika utekelezaji wa klasta ya tatu kuna kamati ambayo wizara zote karibu zinapeleka wajumbe wao, na hawa watu wa MKUZA ndio wanakuwa wenyeviti katika kusimamia zile klasta.

Mhe. Spika, Idara hii ni mratibu wa shughuli za utawala bora. Jukumu hili limeelezwa vyema katika mkakati wa kukuza uchumi na kupunguza umaskini unaofanyiwa mapitio. Katika klasta ya tatu lengo la tatu linaonesha bayana haja ya kuweka na kuimarisha kamati za utawala bora zitakazohusisha watendaji kutoka serikalini na taasisi zisizo za kiserikali. Kamati hii itafanya kazi za kutathmini utendaji na utekelezaji wa utawala bora, kuandaa mipango ya utekelezaji na kutoa ripoti za utawala bora kila mwaka.

Mhe. Spika, suala la *Public Private Partnership* (PPP) ambalo alilizungumza Mhe. Rashid Seif ni muhimu na kwa kweli serikali inalihimiza sana. Sina hakika ni vigezo gani alivyotumia mheshimiwa kuona kwamba *PPP* haipo. Ila namuomba nimtoe wasi wasi kwamba hilo lipo na kwamba serikali inalitilia mkazo. Hata katika kikao cha *business council* kilichofanyika Hoteli ya Bwawani, hili suala lilipewa umuhimu sana na zikaundwa kamati mbali mbali. Pia zilitoa maamuzi mbali mbali ya kujenga mashirikiano baina ya *PPP*.

Mhe. Spika, vile vile alisema kwamba kwa kujibu suala la juu ya barua zinazotolewa na Afisi ya Mufti kwa Waumini kuchangiwa Msikitini. Tunakiri kuwepo kwa jambo hilo. Hii imetokana na ukweli kwamba baadhi ya Waumini hupatwa na matatizo wasiyoyategemea kama vile, wageni wanaokuja Zanzibar wakapoteza mali zao, wanaokuja Zanzibar wasiwakute wenyeji wao na kadhalika.

Pia pamekuwepo na kukwama katika ujenzi wa baadhi ya Misikiti na madrasa. Kwa kutatua shida hizi Afisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar imekuwa ikitoa barua (idhni) baada ya kuthibitisha usahihi wa shida hizo kuruhusu waombaji wapite Misikitini au kwa wafadhili kuomba misaada husika. Tunaunga mkono wazo la mheshimiwa kwa Afisi ya Mufti wa Zanzibar iandae mpango maalum wa utafutaji wa fedha kwa wafadhili wa nje ili kuweza alau kupunguza matatizo haya.

Mhe. Spika, naungana na Mhe. Hija Hassan Hija katika malalamiko yake ya kupinga ubaguzi wa itikadi za kichama katika ndoa. Hakuna popote katika dini ya Kiislamu panapo ruhusu mke kumnyima mume haki yake ya kindoa kwa sababu za tofauti za kichama. Tunatoa wito kwa viongozi wote na wananchi

kwa jumla kuwa waangalifu katika matamshi yetu ambayo yanaweza kupelekea upotoshaji kwa jamii, lakini na hata madhambi kwa Mwenyezi Mungu.

Mhe. Spika, Mhe. Salmin Awadh amezungumzia suala la mgawanyo wa madaraka kwamba haupo na kwa kweli umeathiri utawala bora. Naomba nimtoe wasi wasi kwamba mgawanyo wa madaraka upo, kwani kila mmoja anatekeleza majukumu yake ipasavyo. Tatizo labda ni pale katika suala zima ni mgawanyo wa raslimali kwa maana ya fedha. Katika hili majukumu ya kukusanya mapato imeachiwa muhimili wa kiutendaji. Kwa kweli kwa uhaba wa raslimali zetu lazima tuwe na utaratibu wa kugawana hicho tunachokipata. Hata hivyo tutalichukua na kulizingatia suala hili. Suala hili pia Mhe. Waziri wa Fedha kishaliahidi kwamba kama fedha zitapatikana za kutosha, basi na huu mgawanyo wa kuziwezesha taasisi hizi kufanya kazi zake kwa kujitegemea litatekelezwa. Ni suala zuri katika kutekeleza utawala bora.

Mhe. Spika, kuhusu suala la Mawaziri kukaimu nafasi ya Waziri na ugumu unaojitokeza katika Mawaziri wanao kaimu. Hili kwa kweli halina tatizo, kwani Manaibu Mawaziri wanawajibu kwa mujibu wa Katiba kuendelea kuwasaidia Mawaziri wanaokaimu na wala wajibu wao hauondoki. Kifungu hicho 49(1) kinaelekeza wajibu huo. Hata hivyo tunalichukua wazo lake na litafanyiwa kazi.

Vile vile katika mchango wake Mhe. Mjumbe alizungumzia juu ya Manaibu Mawaziri kuwa Wajumbe wa Baraza la Mapinduzi. Hili ni suala la maamuzi tu, tukiamua wawe hivyo basi watakuwa bila shaka. Lakini kwa bahati Baraza la Mapinduzi lina wajumbe wake na ni idadi maalum haitakiwi kuzidi. Sasa mara nyingi ni kweli anapopewa mtu kukaimu nafasi ya Uwaziri ni kwa sababu hata ukienda mswada kule Baraza la Mapinduzi, yule waziri anayekaimu ndiye anayeupeleka kule. Lakini kazi iliyoko nje ya Baraza la Mapinduzi Manaibu Mawaziri wanatakiwa kufanya.

Mhe. Spika, kuhusu jina la Katibu wa Baraza la Mapinduzi, kuitwa Katibu Mkuu Baraza la Mapinduzi nadhani ni athari za kimazowea na kimamlaka halina tatizo. Aidha, juu ya Katibu Mkuu wa Baraza la Mapinduzi kuwa Kiongozi wa Makatibu Wakuu wote, kikatiba Katibu Mkuu Baraza la Mapinduzi ndio Kiongozi wa Watumishi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, wakati Katibu Mkuu wa Wizara ni kiongozi wa Utumishi katika Wizara yake. Kwa maana hiyo ni wazi kwamba kikatiba Katibu Mkuu ni Mkuu wa watumishi wote serikalini wakiwemo Makatibu Wakuu. Lakini hata hivyo, mheshimiwa asiwe na haraka astahamili kidogo tu, kama litatokea badiliko lolote la Katiba mbele ya safari, nafikiri suala hili litashughulikiwa.

Mhe. Zakiya Omar Juma, katika hotuba yake alitaka kujua mambo yafuatayo. Kesi 2006 za kutoroshwa mtoto Maryam. Hili nimeshalijibu kabisa.

Mhe. Nassor Ahmed Mazrui aliuliza swali kuhusu Mahakama ya Biashara. Suala hili nalo Mhe. Spika, nimeshajibu. Mhe. Said Ali Mbarouk alikuwa na suala la idadi ya mabaa. Nimeshalizungumza vile vile tufanye nini, kwa sababu hata tukipandisha kodi kiasi gani, bado watu wanakuja kukata leseni. Nilisema pale haya mambo ya kishetani haya yana matatizo sana.

Mhe. Spika, mtu anaweza kuwacha kumlisha mkewe na wanawe nyumbani akenda kumlisha mtu wala sio mkewe wala sio mwanawe na akamnunulia nguo na vyakula na kadhalika kwa ajili ya sikukuu, ndio mambo ya kishetani ubaya wake huo. Mwenyezi Mungu atunusuru na mambo hayo. Amina. Lakini yanatokea katika dunia hii hii. Halafu siku ya sikukuu wanawe wakiwa hawakuvaa basi analia na kusema umaskini mbaya, kumbe kishavisha mtu huko. *(Makofi).*

Mhe. Rashid Seif Suleiman aliuliza juu ya vyeti vya kuzaliwa vinachelewa sana mpaka miaka mitatu. Suala hili Mhe. Spika, sisi hatujalibaini kusema kweli, kwa sababu tuna vyeti vingi katika afisi zetu ambavyo havijaja kuchukuliwa. Lakini hata hivyo, tushirikiane zaidi atuletee hii kesi hasa iliyochukua miaka mitatu ili tuweze kutatua hili tatizo.

Mhe. Spika, sisi katika Baraza hili ni watu wamoja, basi ni vizuri kama Mhe. Mwakilishi ana tatizo basi amfuate waziri tu litatuliwe. Wangapi wanatufuata hapa wanakuja na matatizo ya urithi. Mhe. Haji Faki Shaali alikuja na tatizo la urithi hapa, tukalirekebisha mara moja likamalizika. Kwa hivyo, tuwe tunaelezana juu ya masuala na ndio umoja unaotakiwa kujengwa katika Baraza hili. Kesi kama hizi zinaweza zikatokea kama moja au mbili, lakini nyingi zinakuwa zinatekelezwa.

Mhe. Spika, nataka kuzungumza suala la sheria ya rushwa na kuanzishwa kwa Mamlaka ya Kupambana na Rushwa. Suala hili limezungumzwa na Waheshimiwa Wajumbe wengi, akiwemo Mhe. Zahra Ali Hamad ambaye ni Naibu Waziri Kivuli wa Wizara yangu, Mhe. Nassor Ahmed Mazrui na Mhe. Said Ali Mbarouk walizungumza suala hili.

Mhe. Spika, nilipozungumza kwamba Baraza hili limeamua kufanya mafuta na gesi kuwa lisiwe ni jambo la muungano, nilizungumza kwa dhati ya moyo wangu na nikaona kwamba kwa mujibu wa sera ya nishati, kifungu cha 14.7, wizara yangu inalo jukumu hilo na limetajwa wazi kwamba katika masuala hayo Wizara ya Sheria ina wajibu wa kuona kwamba mikataba yote na mambo

mengine yote yanayohusu mambo haya ya mafuta na gesi, basi wizara hii ishughulikie. Katika hicho kifungu cha 14.7.

Mhe. Spika, washauri wa masuala ya mafuta wametoa vitabu hivi ambavyo walitufanyia kwenye semina, na wakatutahadharisha sana juu ya suala la kuhakikisha kwamba tunaposhughulikia mafuta basi kuna mambo tuyatizame kwa uwazi sana. Moja likiwemo rushwa. Humu muna-*chapter* nzima inayohusu masuala ya rushwa katika masuala ya *petroleum*. Sasa hiyo ndio sababu iliyofanya kwamba badala ya huu mswada tukaupeleka bila ya kuingiza kitu hiki, itakuwa sio vizuri.

Kwa hivyo, tuwaombe hawa watusaidie, maana wao ndio wana uzoefu, hizo *corruption* huko, juu ya utoaji wa vibali na mambo mengineyo wanayo mifano. Sisi hatujaingia kwenye mambo hayo hatuna mifano hivyo. Kwa hivyo, watusaidie ili tuingize katika sheria yetu kabisa.

Ndio nikasema kwamba sio kama nilikuwa nabadilisha maneno pale, hapana, nilisema kwamba sheria Nam. 6 ya mwaka 2004, ambayo ni sheria ya makosa ya jinai. Section 76 mpaka 91 inazungumzia suala la rushwa. Kwa hivyo, ikitokea rushwa sasa hivi tuta-*handle* kwa suala hili, wakati tunashughulikia kwenye suala hili la kurekebisha hii sheria lakini hiyo *section* ya 76 mpaka 91 inazungumzia sheria Nam. 6 ya mwaka 2004 inazungumzia rushwa.

Mhe. Spika, na hiki kifungu cha 91 kimetoa uwezo kwa waziri anayeshughulika na masuala ya sheria, ikiwa atahisi kwamba yaliyomo mule ni machache na sasa anataka kuongeza mengine. Katika kanuni zake ndio atalitungia kanuni hilo jambo analotaka kuliongeza.

Hilo jambo halipiti mpaka lililetwa hapa katika Baraza la Wawakilishi kwa sababu ya unyeti wa sheria hii namna inavyofanyakazi kwenye masuala ya rushwa. Sheria hii pia imezungumzia masuala ya ulanguzi, yaani *holding* na mambo mengineyo, kwenye kifungu cha 317. Suala hili nilikuwa natanabahisha wajumbe tu kwamba tuishughulikie hii sheria ili tuingize haya masuala ya mambo ya rushwa katika mafuta, ni hatari sana.

Mhe. Spika, ukenda kwenye mafuta, halafu watu wakatoa vibali bila ya kujali, ni hatari sana na tutaingia kwenye matatizo makubwa sana ambapo tutajua kwa nini tulikuwa tukizungumza haya masuala ya mafuta na kutoa vibali.

Hii ndio sababu tukasema Mhe. Spika, suala hili bora tulishughulikie sisi wenyewe Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa sababu sisi ndio tunaojua bahari na ndio raslimali yetu, anayepata samaki na mambo mengine, ndio maana yake hiyo.

Sasa katika kulishughulikia mimi naanza kwa sababu sina wasi wasi kwamba suala hili litakuwa sio la muungano. Sina wasi wasi na hilo na sina wasi wasi kwa sababu Rais wangu nimeshamsikia kasema hivyo, isipokuwa sasa hivi utekelezaji tu. Sasa nitakuwa na wasi wasi wa nini ikiwa Rais wangu kishasema masuala haya. Kwa hivyo, ni utekelezaji tu sasa hivi ndio unaotakiwa kutekelezwa kwa sababu hii ndio maana nikazungumza suala hili. Kwa hivyo, suala la Mhe. Said Ali Mbarouk kunahusiana na nini. Linahusiana kwamba hili suala ni kuwa linatuhusu sisi moja kwa moja, katika kuhakikisha masuala hayo tunaingiza katika sheria yetu.

Mhe. Spika, sheria ya jinai Nam. 6 sehemu ya 10 inahusu makosa ya rushwa na mambo mengineyo kama nilivyokwisha kueleza.

Mhe. Spika, nimeshazungumza juu ya suala la kuchelewa kwa vyeti vya kuzaliwa. Mhe. Spika, halafu suala la Afisi ya Msajili nalo kuboresha masuala ya usajili, pamoja na kushirikiana na Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar, ambapo Afisi ya Mrajis wa Serikali Zanzibar inaweza kupata kompyuta 10 kwa kupitia Shirika la Maendeleo la idadi ya watu duniani.

Lakini kuna suala la *typewrites* lilitajwa hapa kwamba kwa nini *typewrites* za kuandikia vyeti vya kuzaliwa ni mbovu. Mhe. Spika, tumeshabadilisha hizo *typewrites* karibu katika wilaya zote. Tumeshatoa *typewrites* mpya kwa kazi hizi. Tunaweza tukaja kuandika kwa kutumia kompyuta baada ya kufanikisha baadhi ya mambo fulani ambayo tunahitaji yarekebishwe.

Mhe. Spika, kuna suala la gari la Mrajis. Mhe. Spika, gari Mrajis atapata. Tatizo lililotokea Mhe. Spika, ni kwamba yalipoagizwa magari yale hayakutosha kwa sababu waombaji walikuwa ni wengi, kwa bahati mbaya na Mrajis na yeye akaingia katika wale ambao wako kwenye orodha ya kusubiri, kwa sababu kulikuwa kuna mpango wa kuja magari mengine ili yajazwe kwenye maeneo yale yaliyo kasoro.

Sasa katika bahati mbaya ikabidi zile gari mpaka leo zimechelewa kufika. Hata hivyo, Mhe. Waziri wa Fedha kishaniambia tuendelee na mazungumzo ili tupate gari za Afisi ya Mrajis Unguja na Pemba. Kwa hivyo, mimi nimeshukuru sana kwa kupata kauli hiyo kutoka kwa Mhe. Waziri anayehusika na masuala ya fedha kwamba hili suala tutalishughulikia.

Mhe. Spika, kuna jambo moja sikulitaja katika hotuba yangu lakini nina umuhimu wa kulitaja na kwa kweli nitakuwa mwizi wa fadhila. Ni kuhusu Kamati ya *PAC* namna ilivyoisaidia wizara yangu na ikiwa sikutoa pongezi basi haiyumkiniki. Nawapongeza sana watu wa Kamati ya *PAC* kwa namna wanavyoisaidia wizara yangu. Kwa kusema kweli toka wakati tumeanza na

Mhe. Abass Juma Muhunzi kwa namna alivyokuwa akitusukuma katika kutoa ripoti ndio *petrol* iliyofanya tufike hapa tulipofika leo. Sasa hivi bado tunaendelea na *PAC* kutuhimiza kwamba ripoti ziwe kwa wakati. Kwa hivyo, tunashukuru sana Mhe. Spika, katika suala hili.

Mhe. Spika, kuna suala la wizi wa kompyuta. Mhe. Hija Hassan Hija ameliuliza suala hili. Mhe. Spika, napenda kumridhisha Mhe. Mwakilishi kwamba hili suala mimi nalishukuru sana Baraza hili, hasa katika ripoti za kamati kuweza kulieleza suala lile. Kwa kweli wenzetu polisi sasa hivi wanaliendea mbio na upelelezi unaendelea, na watatujuilisha wamefikia hatua gani. Hii kazi wanaendelea nayo, tumewasiliana nao kwa kweli wametujibu tena kwa barua kabisa, sio kwamba wanatujibu kwa mdomo mtupu. Mhe. Spika, kwa kushirikiana na Baraza ndio tunaweza kufanya mambo mengi kabisa kwa pamoja. Mhe. Spika, saa yangu imekwisha. Kwa hivyo, naomba kutoa hoja.

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Waziri, kwa majumuisho hayo uliyoyafanya. Sasa Waheshimiwa Wajumbe basi niwahoji wale wanaokubaliana na hoja hii ya Makadirio ya Bajeti ya Wizara hii ya Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora, wanyanyuwe mikono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda.

**Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi:** Mhe. Spika, naafiki.

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora:** Mhe. Spika, kwa kuwa Baraza limejadili na kuikubali Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora. Sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili kuvipitisha vifungu vya matumizi ya wizara yangu.

**KAMATI YA MATUMIZI**

**FUNGU 11 -AFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZANZIBAR**

| | | |
|---|---|---|
| Kifungu 02 - | Utawala Unguja | 3,620,000/- |
| | **Jumla ya Fungu** | **3,620,000/-** |

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 14 - MAHAKAMA KUU ZANZIBAR**

| | | |
|---|---|---|
| Kifungu 02 - | Utawala Unguja | 32,000,000/- |
| Kifungu 03 - | Afisi Kuu Pemba | 6,000,000/- |
| | **Jumla ya Fungu** | **38,000,000/-** |

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 33 - WIZARA YA NCHI (AR) KATIBA NA UTAWALA BORA**

| | | |
|---|---|---|
| Kifungu 11 - | Mrajis Mkuu wa Serikali Unguja | 258,250,000/- |
| | **Jumla ya Fungu** | **258,250,000/-** |

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 11 - AFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZANZIBAR**

| | | |
|---|---|---|
| Kifungu 02 - | Utawala Unguja | 909,625,000/- |
| Kifungu 03 - | Utawala Pemba | 237,375,000/- |
| | **Jumla ya Fungu** | **1,147,000,000/-** |

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 14 - MAHAKAMA KUU ZANZIBAR**

| | | |
|---|---|---|
| Kifungu 02 - | Utawala Unguja | 893,220,000/- |
| Kifungu 03 - | Afisi Kuu Pemba | 354,000,000/- |
| Kifungu 06- | Afisi ya Kadhi Mkuu | 143,780,000/- |
| | **Jumla ya Fungu** | **1,391,000,000/-** |

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 15 - AFISI YA MWANASHERIA MKUU ZANZIBAR**

| | | |
|---|---|---|
| Kifungu 02 | -Utawala Unguja | 471,378,000/- |
| Kifungu 05 | -Tume ya Kuchunguza Sheria | 74,622,000/- |
| | **Jumla ya Fungu** | **546,000,000/-** |

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 33 - WIZARA YA NCHI (AR) KATIBA NA UTAWALA BORA**

| | | |
|---|---|---|
| Kifungu 03 - | Afisi Kuu Pemba | 293,608,000/- |
| Kifungu 04 - | Idara ya Mipango na Sera | 25,830,000/- |
| Kifungu 05- | Afisi ya Mufti | 59,239,000/- |
| Kifungu 07- | Kuratibu Shughuli za Utawala Bora | 30,516,000/- |
| Kifungu 09- | Mamlaka ya Kupambana na Rushwa na Maadili ya Viongozi | |

**Mhe. Haji Faki Shaali:** Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii. Katika mchango wangu ambao uliwasilishwa na Mhe. Zahra Ali Hamad niligusia kuhusu Mamlaka ya Rushwa, kutokana na hotuba ya Mhe. Waziri inaonekana hivi sasa tunaachana nayo lakini bado inaombewa fedha.

Kwa kweli hotuba ya Mhe. Waziri inatueleza kwamba sheria ya jinai vimo vifungu vinavyoshughulikia na masuala ya rushwa, kwa hivyo hakuna haja ya kuunda tena chombo hiki. Sasa kwa nini anakiombea fedha.

Mhe. Mwenyekiti, nilipendekeza fungu hili lisiidhinishwe kwa hapa, vyema tukazihamishia sehemu nyengine katika wizara hii niko tayari. Lakini hapa naona hakuna haja ya kuombewa fedha tena.

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora:** Mhe. Mwenyekiti, nasema ni vizuri fedha hizi ziidhinishwe kwa sababu hao wanaofanyakazi hizi ndio wanaotumia fedha hizi ambao wanashughulikia hayo mambo ambayo nimeyaeleza. Kwa mfano, kuwasiliana na masuala ya mafuta na mengine ndio wanafanya hawa, sasa itabidi mambo ya usafiri na mengine.

Kwa kweli rai yake ya kusema ihamishwe hapa na kupelekwa sehemu nyengine nimeifahamu. Lakini ni vizuri kwa sababu tunazo kasma zinazoendelea basi iendelee kubakia hapa, ndio rai yangu mimi *(Makofi)*.

**Mhe. Haji Faki Shaali:** Mhe. Mwenyekiti, tatizo ninaloliona ni kwamba kuomba fedha kwa mamlaka ambayo kila siku hamna hamu nayo, sioni mantiki. Kwa hivyo, ni vyema ingeingia kwenye sehemu ya ruzuku katika mipango na sera ikiwa ni ruzuku kwa hao wanaofanya hiyo kazi, basi ingeeleweka. Lakini hapa inatajwa mamlaka na wala haipo na dhamira ya kuunda hiyo mamlaka hivi sasa haipo.

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Boa:** Mhe. Mwenyekiti, naendelea kusema kwamba sio kama suala la kuunda Mamlaka ya Rushwa limefutwa, bado na litaendelea kufanyiwa kazi. Kwa kweli hakuna sehemu hata

moja kwenye hotuba yetu tuliposema tuachane nayo Mamlaka ya Rushwa. Hivyo, tukiachana na Mamlaka ya Rushwa basi huo si utawala bora hata kidogo, yaani ni vizuri tuwe nacho chombo hiki.

**Mhe. Haji Faki Shaali:** Mhe. Mwenyekiti, nadhani Mhe. Waziri hataki kutuambia ukweli kwa sababu yeye yuko tayari kupambana na rushwa lakini si chini ya mamlaka hii, isipokuwa anatafuta njia nyengine ya kupambana na rushwa, hivyo ndivyo nilivyomfahamu. Lakini tukiangalia kitabu chake inavyodhihirishwa kwamba hii mamlaka kwa hivi sasa hatutaiunda na badala yake tutatumia sheria.

Mhe. Mwenyekiti, nadhani hakuna haja ya kulumbana, tuendelee *(Makofi)*.

| | | |
|---|---|---|
| Kifungu 09 | -Mamlaka ya Kupambana na Rushwa na Maadili ya Viongozi | 13,041,000/- |
| Kifungu 11 | -Mrajis Mkuu wa Serikali Unguja | 7,183,000/- |
| Kifungu12 | -Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali (P) | 60,583,000/- |
| | **Jumla ya Fungu** | **1,730,000,000/-** |

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 35- AFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA**

| | | | |
|---|---|---|---|
| Kifungu 02 | - | Utawala Unguja | 581,900,000/- |
| Kifungu 03 | - | Afisi Kuu Pemba | 137,100,000/- |
| | | **Jumla ya Fungu** | **719,000,000/-** |

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 11 -AFISI YA MDHIIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZANZIBAR**

| | | |
|---|---|---|
| Kifungu 02 | -Utawala Unguja | 1,677,909,000/- |
| | **Jumla ya Fungu** | **1,677,909,000/-** |

*(Vifungu kilichotajwa hapo juu kimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 14 - MAHAKAMA KUU ZANZIBAR**

| | | | |
|---|---|---|---|
| Kifungu 02 | - | Utawala Unguja | 1,561,125,000/- |
| | | **Jumla ya Fungu** | **1,561,125,000/-** |

*(Vifungu kilichotajwa hapo juu kimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 15 - AFISI YA MWANASHERIA MKUU ZANZIBAR**

| | | | |
|---|---|---|---|
| Kifungu 02 | - | Utawala Unguja | 1,718,899,000/- |
| | | **Jumla ya Fungu** | **1,718,899,000/-** |

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 33 -WIZARA YA NCHI (AR) KATIBA NA UTAWALA BORA**

| | |
|---|---|
| Kifungu 04- Idara ya Mipango na Sera | 35,000,000/- |
| Kifungu11-MrajisMkuuwaSerikali(U) | 4,437,720,000/- |
| **Jumla ya Fungu** | **4,472,720,000/-** |

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 35 - AFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA**

| | | | |
|---|---|---|---|
| Kifungu 02 | - | Utawala Unguja | 750,000,000/- |
| | | **Jumla ya Fungu** | **750,000,000/-** |

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

*(Baraza lilirudia)*

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora:** Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora, bila ya mabadiliko. Sasa naomba kutoa hoja Baraza liyakubali makisio hayo.

**Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii:** Mhe. Spika, naafiki.

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, sasa niwahoji wale wanaokubaliana na makisio hayo ya Wizara hii ya Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora wanyanyue mikono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda *(Makofi)*.

**Mhe. Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi**: Mhe. Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, nakushukuruni kwa mashirikiano makubwa ya kuendesha shughuli zetu na kwa kuwa shughuli zimekwisha, basi tukomee hapa.

*(Saa 12:18 jioni Baraza liliakhirishwa hadi tarehe 25/06/2010 saa 3:00 asubuhi)*